
SportPesa
TZS. 517,350,800
CHEZA USHINDE JACKPOT
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**Rugemalira** asimulia siri ya kutonyoa ndevu kwa miaka minne jela

UKURASA 3


TANGAZO
Jumanne Septemba 21, 2021 Nipashe 11

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI

TANGAZO LA NAFASI YA MWENYEKITI WA BODI YA MAJI YA TAIFA

Katibu Mkuu, Wizara ya Maji anatangaza nafasi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Maji ya Taifa. Bodi hii inaundwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka 2009 chini ya Kifungu Na. 20. Muda wa Bodi ni miaka mitatu.

MAJUKUMU YA BODI YA MAJI YA TAIFA
(a) Kuchunguza jambo lolote litakalowasilishwa kwake na Waziri au Wizara ya Sekta nyingine kuhusiana na usimamizi endelevu wa rasilimali za maji na kutoa mapendekezo yao kwa Waziri au Wizara ya Sekta husika, itakavyoona inafaa, kuchukua hatua madhubuti ili kufikia malengo ya Sheria hii;
(b) Kushauri vipaumbele vya uwekezaji na mpangilio wa kifedha na kuratibu na kuunganisha miradi inayotekelezwa kwa fedha za nje na programu zenye kutoa mchango wa kuendeleza rasilimali za maji;
(c) Kushauri katika kujumuisha mipango ya sekta mbalimbali kuhusu tathmini na kupanga rasilimali za maji;
(d) Kushauri uratibu wa mipango ya bonde na usimamizi;
(e) kushauri utatuzi wa migogoro kati ya sekta moja na nyingine na kati ya Bonde moja na lingine;
(f) Kushauri vipaumbele vya uwekezaji na mpangilio wa kifedha;
(g) Kushauri uhamisho wa maji baina ya mabonde;
(h) Kushauri usimamizi wa rasilimali za maji shirikishi,

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI

TANGAZO LA NAFASI YA MWENYEKITI WA BODI YA MAJI YA BONDE LA ZIWA VICTORIA

Katibu Mkuu, Wizara ya Maji anatangaza nafasi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Victoria. Bodi hii inaundwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka 2009 chini ya Kifungu Na. 22. Muda wa Bodi ni miaka mitatu.

MAJUKUMU YA BODI YA MAJI YA BONDE LA ZIWA VICTORIA
(a) Kuandaa mipango ya usimamizi wa rasilimali za maji, miradi, bajeti na mkakati wa utekelezaji wa Bonde;
(b) Kuunganisha mipango ya Wilaya kwenye mipango ya usimamizi wa rasilimali za maji ya Bonde;
(c) Kutoa miongozo na viwango vya ujenzi na matengenezo wa miundombinu ya vyanzo vya maji;
(d) Kufuatilia, kutathmini na kuidhinisha ujenzi na matengenezo wa miundombinu ya vyanzo vya maji;
(e) Kukusanya, kuchakata na kuchambua takwimu zinazohusu usimamizi wa rasilimali za maji;
(f) Kutunza na kuboresha tathmini za upatikanaji mahitaji ya rasilimali za maji;
(g) Kuidhinisha, kutoa na kufuta vibali vya kutumia maji na kutiririsha majitaka;
(h) Kutunza Daftari la Maji kulingana na Kifungu cha 78;

# Nipashe

Jumanne Septemba 21, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580710
www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

UKURASA 11

# Shahidi kesi ya Mbowe afunguka

UKURASA 2



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, akionyesha kitabu maarufu kinachoitwa 'The Power of Positive Thinking' wakati akiingia katika Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Uhujumu Uchumi jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

UKURASA WA 4

## WAVAMIA MSAFARA WA CCM KILIO CHA MAHINDI

ZAIDI ya wakulima wa mahindi 243 wamelalamikia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA), kutonunua mazao yao kama ilivyoelekezwa na serikali, huku wengine...



UKURASA WA 7

## WAGOMBEA 10 UPINZANI WAENGULIWA UDIWANI

WAGOMBEA 10 kutoka vyama vya upinzani, wameenguliwa kuwania udiwani wa Kata ya Ndembezi Manispaa ya Shinyanga, kwa madai...

UKURASA WA 7

## UTOUH ATAJA KIKWAZO KWA WAKAGUZI WA NDANI

ALIYEKUWA Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali(CAG), Ludovick Utouh, amesema bado kuna tatizo kubwa kwa viongozi ...



# 'Ipo rushwa upandishaji madaraja kwa walimu'

UKURASA 3

# Polisi aliyemuua Hamza apewa tuzo

UKURASA 2

MICHEZO NABI AMTAJA MAYELE, DJUMA SIMBA, YANGA UK.24
MAONI, KATUNI UK.6

# Shahidi kesi ya Mbowe afunguka

**Na Kulwa Mzee**

INSPEKTA Mahita Omari ameieleza mahakama kuwa madai kwamba mshtakiwa, Adamu Kasekwa alifungwa jaketi usoni kuanzia Moshi hadi Dar es Salaam, siyo kweli kwa kuwa hakuruhusiwa kufanya hivyo.

Shahidi huyo wa pili wa kesi ndogo katika kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe na wenzake watatu alitoa ushahidi huo jana Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi mbele ya Jaji Mustapha Siyani.

Akihojiwa na Wakili wa Utetezi, Peter Kibatala, kuhusu madai kwamba mshtakiwa wa pili, Kasekwa aliteswa kabla na wakati anachukuliwa maelezo, Mahita alidai hawaruhusiwi kufanya hivyo.

Wakili Kibatala alihoji kama wanapokuwa katika mahojiano wanaruhusiwa kuwa na bisibisi kumtisha mtuhumiwa atoe maelezo.

Pia, Kibatala alidai kuna taarifa pia mshtakiwa alichomwachomwa na bisibisi huku akiambiwa kama hatatoa maelezo wanayotaka wao watamfanyia walichofanya wakiwa Moshi.

Inspekta Mahita alidai hayo yote hayaruhusiwi kufanyiwa mtuhumiwa na kwamba katika ukamataji walipata ushirikiano kutoka kwa washtakiwa.

Wakili Kibatala alihoji kama Polisi wanaruhusiwa kumfunga pingu mtuhumiwa mikononi na miguuni kisha kumning'iniza kama mshkaki huku wakimpiga kwenye nyayo.

Shahidi alihojiwa kama wanaruhusiwa kumfunga jaketi mtuhumiwa kutoka Moshi hadi Dar es Salaam.

Inspekta Mahita alikanusha tuhuma hizo na kudai kwamba hakukuwa na haja ya kumfunga jaketi, hawakumtesa kwani hawaruhusiwi.

Akihojiwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Pius Hillar, kuhusiana na ushahidi wake, aliendelea kusikiliza kwamba polisi hawaruhusiwi kumtesa mtuhumiwa.

Alidai Moshi waliishi katika mazingira mazuri na washtakiwa, waliwapa ushirikiano hadi wanafika nao Dar es Salaam.

Shahidi wa pili alimaliza kutoa ushahidi aliingia shahidi wa tatu, Koplo Msemwa ambaye alidai Agosti 7, mwaka jana alikuwa zamu Kituo cha Polisi cha Kati Dar es Salaam, alikuwa na jukumu la kutunza mahabusu.

Anadai alikabidhiwa mahabusu saa kumi na mbili kasoro asubuhi, alienda kuwahakiki kama idadi aliyokabidhiwa ndio hiyo na akiwa huko alimwona Kamishna Msaidizi wa Polisi, Ramadhan Kingai akiingia akiwa na ASP Jumanne na watuhumiwa wawili.

Msemwa akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Nassoro Katuga, anadai ACP Kingai alikuwa na askari wengine waliovaa kiraia wakiwa wameshika bunduki na watuhumiwa walikuwa na pingu mikononi, alipewa namba ya jalada akaona ni kesi ya kula njama kufanya vitendo vya kigaidi.

Aliwataja washtakiwa aliokuwa nao Kingai kuwa ni Adamu Kasekwa na Mohammed Ling'wenya, aliwapokea na kuwaingiza katika kitabu cha kumbukumbu na kuwapekua kama wanakitu chochote ambacho hawaruhusiwi kuingia nacho mahabusu.

Anadai Kasekwa alikuwa na jaketi, alipomuhoji alisema afya yake nzuri na Ling'wenya pia alisema afya yake iko vizuri.

Anadai Kasekwa aliingia mahabusu saa 12.09 asubuhi na saa moja na dakika kumi na moja ACP Kingai alimwagiza akamtoe nje anataka kwenda kumuhoji, shahidi alimtoa wakaelekea ofisi ya Mkuu wa Upelelezi Mkoa.

Anadai alirudishwa saa tatu na dakika tano na Mrakibu Msaidizi wa Polisi Jumanne alimchukua Ling'wenya saa mbili na dakika kumi kwa ajili ya upelelezi na alirudi saa tano na dakika sita asubuhi Agosti 7, mwaka jana.

Shahidi anadai baada ya kumaliza zamu hakuwaona tena washtakiwa, katika kitabu cha kumbukumbu kilichopokelewa kama kielelezo mahakamani inaonyesha Agosti 8, mwaka jana walitolewa mahabusu kwa ajili ya upelelezi.

Alipotakiwa kusema kama akiwaona anawajua ama la, shahidi anadai anawajua, alikuwa makini nao kutokana na tuhuma zao za kulanjama kufanya vitendo vya kigaidi kwani tangu aingie Jeshi la Polisi mwaka 2013 hajawahi kusikia tuhuma kama hizo.

Anadai watuhumiwa wakiwa kituoni walikunywa uji asubuhi, mchana walikula ugali na maharage na jioni pia walipewa chakula.

Akihojiwa na Wakili wa Utetezi, Jeremiah Mtobesya, kama waliwapeleka hospitali watuhumiwa baada ya kuwapokea, alidai mtuhumiwa hupelekwa hospitali baada ya kujieleza kuhusu afya yake, akisema mgonjwa anapelekwa.

Watuhumiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, Kasekwa, Ling'wenya na Halfani Bwire ambao wanatuhumiwa kwa mashtaka sita yakiwamo ya kula njama kufanya vitendo vya kigaidi.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akikagua ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Karagwe baada ya kuweka jiwe la msingi la ujenzi wake akiwa katika ziara ya kikazi Mkoa wa Kagera mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Naibu Waziri TAMISEMI (Elimu), David Silinde. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Polisi aliyemuua Hamza apewa tuzo

**Na Maulid Mmbaga**

POLISI aliyemuua Hamza Mohamed, Askari Mashaka Masinde na wenzake 10 wametunukiwa tuzo ya heshima na ujasiri.

Lengo la tuzo hiyo ni moja ya kutambua mchango wao katika kuimarisha ulinzi na usalama nchini.

Akizungumza jana kwa niaba ya Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP) Simon Sirro, Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Muliro Muliro, wakati wa hafla ya kuwatunuku, alisema kazi ya polisi ni miongoni mwa kazi ngumu tofauti na watu wanavyozitazama.

Pia, alisema kwa mujibu wa katiba, jukumu alilopewa polisi ni kubwa ikiwamo kulinda wananchi pamoja na mali zao.

Alisema kuwa baadhi ya polisi wengine walipoteza maisha wakiwa wanatimiza majukumu yao, ili kuhakikisha kuwa madhara makubwa hayatokei.

"Mimi nikiwa kama kamanda wa polisi nawapongeza askari wote waliopambana na vitengo vyote kwa kazi kubwa ya weledi waliyoifanya, kwa sababu kama ingekuwa kazi ya ovyo watu zaidi wasiokuwa na hatia wangepoteza maisha.

"Pia niendelee kuwatia moyo wale askari wetu jasiri ambao wameumia wakati wa utekelezaji wa majukumu yetu... pia niendelee kuwatia moyo familia za askari walipoteza maisha kwa niaba ya watu wengine, kwani hizo ndizo kazi za askari na vita dhidi ya wahalifu inaendelea," alisema Muliro.

Aliongeza kuwa IGP Simon Sirro amewatambua kimaandishi polisi wote waliowawakilisha katika tukio la kupambana na Hamza, pia mtizamo wa kisayansi wa kushughulika na matendo ya kihalifu ni kuyazuia, na alidai kuwa hawafurahi matukio yatokee ndiyo waende kwenye upelelezi.

"Tunataka tuwajue wahalifu tuwazuie kabla hawajatenda vitendo vya kiuhalifu, ndio maana tunahimiza kutoa taarifa za kihalifu ili sisi tuwakamate kabla hawajatekeleza azma yao, na huo ndio mtazamo wa kijeshi wa kanda maalum," alisema Muliro.

Aliongeza kwa kulitaka Jeshi la Polisi kuendelea kutii sheria, maadili na kanuni za jeshi hilo kwa kujiepusha na vitendo ambavyo vinakiuka maadili ya utendaji wa jeshi ili kuendelea kujenga imani kwa wananchi na kazi yao iweze kuwa rahisi.

Kwa upande wake, Masinde aliwataka maofisa wa usalama kujitoa kwa moyo mmoja na kuendeleza jitihada za kupambana na wahalifu kwa muda wote, ili kulinda amani ya nchi bila kujali jambo lolote.

"Askari wote tujitoe kwa moyo mmoja, tuendelee kupambana na wahalifu kwa muda wote bila kujali kuwa kuna hili limetokea," alisema Masinde na kuongeza:

"Polisi tuwe na ujasiri tusiogope hata kama utaona mwenzio kauawa wewe songa mbele, kwani ndiyo kazi tuliyo apa kuifanya."

# Mamia wamuaga mke wa Mrema

**Na Waandishi Wetu**

MAMIA ya waumini, wanasiasa na viongozi wengine jana, waliungana na familia ya Mwenyekiti wa TLP, Augustine Mrema, kumuaga mkewe, Rose Mrema (67), aliyefariki dunia Septemba 15, mwaka huu.

Baadhi ya wanasiasa waliohudhuria ni Mbunge wa zamani wa Jimbo la Moshi Vijijini, Thomas Ngawaiy; Mwenyekiti wa UDP, John Cheo; Mwakilishi wa ACT-Wazalendo, Jane Nchimbi na aliyekuwa mgombea urais wa TLP mwaka 2020 na viongozi wengine wa dini.

Ibada ya kuaga mwili wa Rose, ilifanyika katika Parokia ya Mtakatifu Augustino, Salasala Dar es Salaam na katika mahubiri yake Paroko Peter Asenga, aliwataka waumini kujifunza kupitia kifo cha Rose, kuandaa maisha ya baada ya kifo kwa kuishi kwa hofu ya Mungu muda wote.

Naye Ngawaiya alisema, "Rose alikuwa msaada mkubwa kwangu hasa kipindi cha uchaguzi, kwani aliweza kuhamasisha wananchi kunipigia kura, hakuwa mwanasiasa, lakini alifanya shughuli za kisiasa kutusaidia TLP wakati huo," alisema.

"Huyu mama alikuwa mzalendo, mchakapazi, mweye upendo na mcha Mungu. Alijali sana... nakumbuka alionyesha upendo hasa walipopitia hali ngumu na mumewe, nilishuhudia wakati tulipolazwa wodi moja na mumewe nchini India, "alisema Cheo.

Naye Mrema aliwataka Watanzania kuishi kwa umoja na mshikamano, kama alivyokuwa akiishi mkewe.

"Mke wangu hakuwa mbaguzi, alimpenda kila mmoja alishirikiana na mimi kwa dhati katika shughuli za ujenzi wa nchi, hakuwa mwenye majivuno," alisema Mrema.

**Imeandikwa na Paulina Chimeledya, Ally Mlanzi na Kalebo Mussa**

## Bidhaa zilizofungashwa kuhakikiwa mipakani Okt.

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

WAKALA wa Vipimo Mkoa wa Kigoma unatarajia kuanza uhakiki wa bidhaa zilizofungashwa mipakani Oktoba mwaka huu baada ya kushindikana kufanyika kwa takribani miaka 10 kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo upungufu wa watumishi.

Akielezea namna zoezi la uhakiki wa bidhaa mipakani litakavyofanyika, meneja wa Wakala wa Vipimo Mkoa wa Kigoma, Laurent Kabikiye, alisema uhakiki utafanyika katika mipaka rasmi na wataanza na maeneo mawili ya Bandari ya Kigoma na Kibirizi na kutaka wafanyabiashara wajiandae kuwasilisha sampuli.

Kuhusu kuchelewa uhakiki wa bidhaa katika mkoa huo, alisema kumesababishwa na upungufu wa watumishi kwa muda mrefu na kwa sasa kuna maofisa vipimo sita ambao wataweza kusimamia katika maeneo mawili wakati taratibu za kuongeza watumishi zikiendelea kufanywa na makao makuu.

Alisema watatumia vyombo vya ulinzi na usalama kama wadau wakuu ili kuhakikisha bidhaa zote za biashara zinapitia katika mipaka rasmi kutokana na mkoa wa Kigoma kuwa na mipaka mingi isiyo rasmi na mwingiliano mkubwa Watanzania na nchi jirani.

Hussen Kinga, Mwenyekiti wa Chama cha Mawakala wa Forodha Kigoma, alisema wadau wengi hawana uelewa wa zoezi hilo kwa kuwa ni geni kwao na wanapaswa kuzidi kuwakutanisha na kutoa elimu itakayo saidia kuongeza ufanisi wa kazi.

"Watu wa vipimo tunaomba waainishe vipimo mbalimbali kama urefu, ujazo na upana kwa ufasaha ili kuondoa mkanganyiko," alisema.

Uhakiki huo utadhibiti udanganyifu wa uuzaji bidhaa zilizofungashwa zisizo endana na thamani ya fedha na kuwezesha serikali kukusanya mapato kwa ufanisi kulingana na uhalisia wa bidhaa.

# TAMISEMI yabaini rushwa upandaji madaraja walimu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

OFISI ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imebaini kuwapo kwa vitendo vya rushwa katika upandishaji wa madaraja ya walimu na kuagiza Tume ya Walimu nchini (TSC) kudhibiti suala hilo.

Pia, imeagiza kufanyika kwa tathmini na kuona ni idadi gani ya walimu ambao wanastahili kupandishwa daraja ili suala hilo lifanyiwe kazi kwa haraka.

Naibu Katibu Mkuu wa ofisi hiyo, anayeshughulikia elimu, Gerald Mweli, aliyasema hayo jana alipokuwa akifungua mafunzo kwa walimu jijini hapa.

"Nisingependa kuona hizi Sh. 50,000 zinatumika kuwadai walimu ili majina yao wapelekwe katika upandishwaji madaraja, ninachohitaji kuona ni haki inatendeka."

Alisema rushwa ni adui wa haki na haipaswi kuendekeza na kuwataka kufanya kazi kwa bidii na kupeleka majina ya wanaostahili kupandishwa madaraja.

"Nawaomba suala la rushwa mliweke pembeni haki itendeke katika hili la upandishwaji madaraja," alisema Mweli.

Alisema hakuna sababu ya kunyanyasika kazini kwa kuwa Tume hiyo ipo kwa ajili ya kutekeleza wajibu wake.

"Serikali haitakuwa tayari kumvumilia mtu yeyote ambaye atabainika anafanya vitendo vya rushwa hatua kali dhidi yake zitachukuliwa," alisema.

Alisema kuna walimu wengi wanastahili kupandishwa vyeo wafanye hivyo ili wazidi kufanya kazi kwa bidii na kuipandisha sekta ya elimu nchini.

Naye, Katibu Mtendaji wa TSC, Paulina Mkwama, alisema washiriki wa mafunzo hayo ni kutoka mikoa ya kanda ya kati ambayo ni Dodoma, Iringa, Singida na Manyara.

Alisema mafunzo hayo yanatolewa ili kuwezesha kamati hizo kutekeleza majukumu yao ipasavyo na kwa weledi katika kushughulikia haki za walimu.

Awali, Mwenyekiti wa Tume hiyo, Willy Mbogo, aliwataka washiriki wa mafunzo hayo kuwa makini katika mafunzo hayo ili kuboresha utendaji wao.

## Rugemalira asimulia siri kutonyoa nywele miaka 4



**Na Donald Lukele,** TUDARCo

MFANYABIASHARA James Rugemalira juzi alieleza Kanisa Katoliki, Parokia ya Makongo Juu, Dar es Salaam kuwa hajanyoa ndevu wala nywele za kichwani kwa miaka minne na miezi mitatu alipokuwa chini ya mamlaka za dola.

Akizungumza katika ibada ya shukrani katika kanisa hilo alililojenga kwa kushirikiana na waumini wenzake, alisema "Hizi nywele sijawahi kuzinyoa tangu nilivyoingia gerezani, baby (mke wangu) alitaka kuninyoa ila nilivyokuja kushukuru nilimwomba Paroko amwambie asininyoe, nimeziacha hivi kwasababu, hivi nilivyo kunaongea, sina la kuongea zaidi."

Rugemalira ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya IPTL, alisema lengo la kwenda kanisani humo ni kumshukuru Mungu kwa kumtetea kauli iliyoungwa mkono na Mkewe Benedicta ambaye alisema ni maombi kama ya Paulo na Sila yamemwezesha mpendwa wao kutoka gezerani.

Aidha, aliwashukuru waumini kwa sala na kumtembelea gerezani kwa kipindi chote alichokuwa gerezani.

"Kiukweli niwapongeze kwa hatua kubwa iliyofanyika, kuwa na Hekalu la Bwana la aina hii yaani naona maajabu kila nikiangalia huku na kule, hongereni sana," alisema Rugemalira.

Akizungumza baada ya mfanyabiashara huyo kushukuru, Paroko wa Jimbo hilo Joseph Massenge, alimpongeza kwa msimamo na kwamba hakika ushujaa wake ni mfano wa kuigwa kwa waumini hao.

"Huu ndiyo ukristo wa kweli mnatakiwa kuiga mfano wa maisha haya mjitoe sadaka kwa kusimamia ukweli kama unahisi unasimamia ukweli," alisema paroko.

Aidha, aliisifu imani ya Rugemarila baada ya kitendo cha kuchagua kufika kanisani hapo baada ya kutoka mahabusu kwa takribani miaka minne ambayo ni imani kubwa na ya mfano, huku akimsihi kusamehe yote na kuanza maisha mapya yasiyo na kinyongo wala kulipiza kisasi kwani huo ndio ukristo wa kweli.

Rugemarila aliachiwa Septemba 16, mwaka huu, baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kuwasilisha hati ya Nole chini ya kifungu cha 91(1) kuwa hana nia ya kuendelea na mashtaka yanayomkabili mtuhumiwa huyo.

Rugemalira alikuwa akikabiliwa na mashtaka 12 ikiwamo ya utakatishaji wa fedha na kusababisaha hasara ya dola za Marekani 22,198,544.6 na Sh. 309,461,300,158.27..




# Wavamia msafara wa CCM kulalamikia mahindi

**Na Beatrice Shayo,**
ALIYEKUWA RUVUMA

ZAIDI ya wakulima wa mahindi 243 wamelalamikia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA), kutonunua mazao yao, kama ilivyoelekezwa na serikali, huku wengine wakisota kwa zaidi ya mwezi mmoja, bila kujua hatima ya malipo yao.

Wakulima hao walitoa kilio hicho jana mbele ya viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka, aliagiza wakala huyo kulipa fedha hizo kwa kuwa serikali ilishazitoa.

Akiwasikiliza wakulima hao, ambao waliingia kwenye msafara wa viongozi wa CCM, walimlalamikia kukaa kwenye ghala la kuhifadhi mahindi kwa zaidi ya mwezi, bila bidhaa zao kununuliwa licha ya serikali kutoa fedha, alisema ni muhimu utekelezaji ukafanyika haraka.

Nasoro Nyoni, ambaye anasubiri mahindi yake kununuliwa alisema hawajui hatma ya mahindi yao kwa kuwa wanapoteza muda mwingi kufuatilia malipo yao, bila muafaka.

Alisema wamepatiwa taarifa ya serikali kutoa fedha, kwa ajili ya ununuzi wa mahindi, lakini kwenye utekelezaji hakuna.

"Nipo hapa tangu Agosti 15, mwaka huu, nasubiria mahindi yangu yanunuliwe na yanavyochelewa yanaanza kuliwa na mchwa, pia tunapoteza muda mwingi kukaa hapa," alisema Nyoni.

Naye, Saimon Rwiga alisema ana mwezi tangu ayalete mahindi yake na anashindwa kuondoka kwa kuwa anasubiria malipo yake, ili aweze kufanya shughuli nyingine.

Pumziko Philemon, alisema anachokiona ni kama serikali haikuwa na fedha za kununua mazao, hali ambayo imesababisha usumbufu unaoendelea.

Alisema awali zilikuwa tani 1470 za mahindi yakauzwa tani 1,000 na kubaki tani 470, ambazo ziliuzwa kwa wale wenye mahindi kuanzia magunia 80.

Philemon alisema iliwalazimu kujiorodhesha wale wote, ambao wamewasilisha mahindi yao, kwa ajili ya kununuliwa na idadi walifika 243.

Alisema lengo la kujiorodhesha, ili watakaoleta mahindi yao yafuate utaratibu wa namba yatakapokuwa yananunuliwa, jambo ambalo halikuweza kufanikiwa.

Shaka baada ya kuwasikiliza wananchi hao aliwaomba wamsubiri kwa muda mfupi, kwa ajili ya kwenda kufanya kikao cha dharura na Meneja wa Kanda NFRA, Ramadhani Nondo, mbunge na mkuu wa wilaya, ili amueleze ni kwa nini jambo hilo limetokea.

Shaka aliitaka NFRA kuweka utaratibu mzuri, ili kumaliza sintofahamu iliyopo juu ya ununuzi wa mahindi, Manispaa ya Songea kwa kuhakikisha wananchi wote waliokwisha orodheshwa, mahindi yao yananunuliwa.

Alisema NFRA waongeze kituo kimoja cha ununuzi wa mahindi, ili kuepuka msongamano katika kituo kinachotumika sasa na kuwaondolea wananchi usumbufu.

"Serikali ya CCM inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan imetoa Sh bilioni 7.5, kwa ajili ya ununuzi wa tani 35,000 katika hatua za awali kwa NFRA hapa Songea mjini na fedha hizo tayari zipo kwenye akaunti zao, chama kinaitaka NFRA kutoa kipaumbele kwa wananchi wote waliokwisha kuorodheshwa," alisema.



Aliyekuwa mgombea ubunge Jimbo la Mkuranga mkoani Pwani, kwa tiketi ya ACT-Wazalendo, Mohamed Mtambo (wapili kushoto), akimpa kadi ya uanachama wa chama hicho aliyekuwa Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kata ya Dondo, Abassi Ndambwe (wapili kulia) aliyejiunga na chama hicho. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

## PM: Tutakuza uchumi wa mtu mmoja mmoja

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema mkakati wa serikali ya awamu ya sita ni kuboresha na kukuza uchumi wa mwananchi mmoja mmoja, hivyo kila Mtanzania afanye kazi kwa bidii.

"Sasa tunakwenda kusimamia maboresho ya uchumi wa mtu mmoja mmoja, Watanzania wote kila mmoja katika eneo la migodini, viwandani, wavuvi, wakulima, wasomi na wafanyabiashara wafanye kazi kwa bidii ili kujiongezea tija."

Ameyasema hayo juzi wakati akizungumza na wananchi, baada ya kukagua ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) kilichoko wilayani Karagwe, mkoani Kagera akiwa katika ziara ya kikazi ya kukagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika mkoa huo.

Majaliwa alisema katika kuhakikisha mkakati huo unafanikiwa, Rais Samia Suluhu Hassan ametoa fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa vyuo vya VETA katika kila halmashauri. Vyuo hivyo vinatoa mafunzo mbalimbali yatakayowawezesha vijana hao kujiajiri au kuajiriwa.

Alisema mafunzo hayo ambayo yatakuwa yanatolewa katika taaluma za TEHAMA, ufundi umeme, makenika, ushonaji nguo, utawawezesha vijana wa Kitanzania kujiajiri au kuajiriwa. "Hatua hii itawakwamua kiuchumi na kuwaondoa katika utegemezi, huu ndio mkakati wa Rais Samia."

Hata hivyo, Majaliwa ameonyesha kutoridhishwa na kasi ya ujenzi wa mradi huo ambao unagharimu shilingi bilioni sita na kumuagiza mkandarasi anayejenga ambaye ni Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ahakikishe anaukamilisha kwa wakati ili malengo ya serikali yaweze kutimia.

Mradi huo unahusisha ukarabati majengo matano na kujenga majengo mapya manane ambayo ni kubadilisha jengo la utawala kuwa madarasa, kukarabati karakana ya ushonaji, kubadilisha jengo la bohari na kuwa karakana ya ufundi wa zana za kilimo na ufundi bomba.

Pia, kubadilisha bohari ya vitu vya jumla kuwa karakana ya uchomeleaji na uungaji vyuma kukarabati karakana ya ufundi wa magari.

# Polepole ashauri umakini uhamishaji machinga

**Na Enock Charles**

MBUNGE Humphrey Polepole ameshauri kuwapo kwa umakini katika suala la kuwahamisha wafanyabiashara wadogo maarufu 'Machinga' katika maeneo ya barabarani.

Amesema lazima kwanza ijulikane hatima ya watakapopelekwa kwa kufanya uchambuzi wa kina.

Akizungumza katika darasa lake la mtandaoni, Polepole ambaye aliwahi kuwa Katibu Mwenezi wa CCM Taifa, alisema ni vyema kuzingatia uchambuzi wa wadau kuhusu uhakika wa soko katika maeneo watakapowahamishia machinga.

"Kuhusu habari ya wamachinga tuwe 'very carefully' (makini) na hii 'issue' (suala) kwa sababu ukikurupuka tu na hii issue inakwenda vibaya lazima tu 'apply' sayansi kwenye jambo hili kwa nini watu wapo barabarani kwa mfano usiwahamishe mpaka wamekujibu kwanini wapo barabarani, hapa nazungumzia uchambuzi wa wadau," alisema Polepole.

"Halafu waulize eti nikikutengenezea soko mahali fulani utakwenda au huendi atakupa sababu za kwenda atakupa kwa maana ya zile nzuri na mbaya halafu wewe utaangalia je inawezekana kumpeleka kule sasa kwa mazingira ya sasa hivi," alisema.

Wiki iliyopita Rais Samia Suluhu akiwaapisha mawaziri Ikulu, jijini Dodoma aliagiza wakuu wa wilaya na mikoa nchini kuwapanga vyema na kuonya anayoyaona kwenye runinga ya ngumi, kupigana, kufukuzana, kuchafuliana na vitu kumwagwa, hataki kuyaona.

"Niwaombe sana ndugu zangu wakuu wa mikoa mnaonisikia na wale wanaonisikia kupitia runinga wachukue hatua zinazostahiki bila kuleta vurugu, fujo na uonevu," alisema.

Alitoa wito kwa machinga au wajasiriamali wafuate sheria na kanuni zilizopo na wajitahidi kufuata yale wanayopangiwa na wakuu wa mikoa na wilaya.

Tayari katika Jiji la Dar es Salaam mabango ya kutangaza kuwaondoa machinga walioweka vibanda juu ya mifereji ya maji, njia za wapita kwa miguu, hifadhi za barabara na mbele ya maeneo ya taasisi za umma kama shuleni yamewekwa ili kutoa tahadhari kwa wafanyabiashara wanaofanya shughuli zao katika maeneo hayo.

# TANGAZO

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## MAOMBI YA TAARIFA YA KUONYESHA NIA YA KUTOA HUDUMA YA TEHAMA PAMOJA NA VIFAA VYA TEHAMA KUMBUKUMBU NA. 10007040

TotalEnergies East Africa Midstream B.V. (Kampuni) Tanzania, kampuni ya kimataifa ya nishati, inaalika makampuni/taasisi yenye sifa na uzoefu katika kutoa huduma pamoja na vifaa vya technolojia ya Habari na mawasiliano katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha Mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta hayo katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni karibia kilomita 1,443, kati hizo kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania. Uendelezaji wa Mradi wa EACOP unahusisha uandisi wa kina, ujenzi, uendeshaji na uboreshaji wa miundombinu ya Mradi.

**MAELEZO MAFUPI YA MAWANDA YA HUDUMA:**

Ili kutekeleza majukumu yake, Kampuni inahitaji huduma kutoka kwa wakandarasi wenye uzoefu na sifa nzuri katika kutoa huduma za miundombinu ya mawasiliano pamoja na huduma za mfumo wa kompyuta ikiwemo utatuzi wa changamoto. Huduma zinazotarajiwa ni:

- Utoaji wa huduma za vifaa: kompyuta na mfumo wake, simu na vifaa vinavyoambatana na matumizi ya simu, kufunga mfumo wa umeme na mawasiliano (cabling), mtandao, mfumo wa kuhifadhi taarifa (server) na vifaa vinavyohusiana na huduma hizi.
- Mafunzo kwa timu ya watendaji na watumiaji.
- Huduma za ziada za ushauri (kama vile uundaji, usimamizi wa mfumo, pamoja na ukaguzi).
- Huduma za mawasiliano ya simu.
- Huduma za usaidizi katika uendeshaji pamoja na marekebisho.

**Kama ilivyo katika matakwa ya Kampuni katika vipengele hivi:**

- Kipengele cha kwanza: miundombinu ya mtandao iliyojikita kwenye mfumo wa Cisco.
- Kipengele cha pili: mfumo wa uhifadhi taarifa (server) uliojikita kwenye mifumo ya Microsoft Azure na NetApp.
- Kipengele cha tatu: Mfumo wa kompyuta binafsi uliojikita kwenye mfumo wa Windows, Android na simu za iOS, Microsoft Office 365 na Azure.
- Kipengele cha nne: Mfumo wa usalama mtandaoni.
- Kipengele cha 5: Huduma za kuchapisha.
- Kipengele cha 6: huduma za mawasiliano ya simu.
- Kipengele cha 7: Mfumo wa moja kwa moja (fixed) wa kupata huduma za mtandao.

**VIGEZO MUHIMU:**

Makampuni au taasisi zinazoonyesha nia zinatakiwa kuwasilisha taarifa za:

- Uwezo wa kifedha wa kutekeleza mkataba.
- Uthibitisho wa uzoefu wa kutoa huduma tajwa.
- Uzingatiaji wa Kanuni za Maudhui ya Wazawa za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Wazawa (Nafasi za Ajira na Huduma kwa Watanzania.
- Usajili katika Kanzi Data ya Watoa Huduma wa Ndani ya EWURA (LSSP) katika kipindi cha kuwasilisha nia kwa ombi hili yanahimizwa.
- Mkandarasi LAZIMA awe na cheti cha ushirika cha watendaji/watoa huduma katika soko.

Makampuni yenye nia, uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com (ukubwa usiozidi MB20)** kichwa cha habari kikiwa ni kumbukumbu namba husika hadi kufikia saa **11:00 jioni Majira ya Afrika Mashariki,** tarehe **27 Sept. 2021** Makumpuni yaliyokidhi vigezo muhimu pekee ndiyo yatakayopata fursa ya kuwekwa kwenye orodha ya makampuni ya awali yenye vigezo.

216462801

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## OMBI LA TAARIFA YA KUONYESHA NIA (EOI) KWA AJILI YA KUTOA HUDUMA ZA USHAURI WA MAZINGIRA NA UWIMAMIZI NA URATIBU WA TAKA KUMBUKUMBU NA. 10007040

TotalEnergies East Africa Midstream B.V (Kampuni) Tanzania, kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi, inaalika makampuni yenye utaalamu na uzoefu katika kutoa Huduma za Ushauri wa Kimazingira na kushauri kuhusu Usimamizi na Uratibu wa Taka, kutuma nia ya kutoa huduma katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA MAWANDA YA HUDUMA:**

Kampuni inahitaji huduma kutoka kwa makampuni yaliyobobea katika kutoa huduma za Ushauri wa Mazingira na kushauri kuhusu kipengere maalumu cha Usimamizi na Uratibu wa Taka na kitahusisha:

- Utambuzi wa namna ya kuepuka na kupunguza uzalishaji wa taka katika maeneo ya kazi hatakabla ya kufikiria usimamizi wa taka hizo nje ya Mradi.
- Utambuzi na ukaguzi wa wakandarasi wa wa taka kuanzia katika ngazi ya eneo husika, wilaya, mkoa na taifa, kutathmini miundo mbinu ya taka na fursa zinazofaa ili kukidhi mahitaji ya ujenzi wa Mradi.
- Kufanya ukaguzi wa Usalama wa Afya na Mazingira kwa wakandarasi wa kusimamia uchafu pamoja na miundombinu ya uchafu.
- Ubainishaji wa kina wa usimamizi wa taka uliojikita katika makadirio ya taka zitakazozalishwa na Mradi pamoja na suluhisho la mwisho la usimamizi wa taka hizo.
- Uboreshaji (Marudio) wa Mkakati wa Usimamizi wa Taka.

**VIGEZO MUHIMU:**

Makampuni au mashirika yatakayoonesha nia, yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Uzoefu, utendaji, na uwezo katika kutoa huduma za ushauri wa masuala ya mazingira na hasa majukumu yaliyotajwa hapo juu katika usimamizi wa taka katika Miradi Mikubwa nchini Tanzania, na kwa kuzingatia viwango vya kitaifa na Kimataifa ikiwemo viwango vya Shirika la Kimataifa la Fedha (IFC). Kampuni iwe na uzoefu/utendaji usio wa chini ya miaka 5 kwa hapa nchini Tanzania au hata Kimataifa, katika kutoa huduma zote zilizoainishwa.
- Kuwa na wafanyakazi viongozi na wenye kukidhi vigezo na wazoefu katika ukaguzi wa masuala ya Afya, Usalama na Mazangira katika miundombinu ya kusimamia taka katika miradi ya mafuta na gesi inayozingatia vigezo vya kimataifa vya Shirika la Fedha (IFC).
- Uwezo wa kifedha kuweza kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha mahesabu ya fedha ya mwaka 2020.
- Usajili katika Kanzi Data ya Watoa Huduma Wazawa ya EWURA (LSSP) katika kipindi cha kuwasilisha nia kwa ombi hili yanahimizwa.
- Uthibitisho wa sera ya kampuni ya Ubora, Afya, Usalama Kazini na Mazingira (QHSE), taratibu na mchakato unaozingatia viwango vya nchi husika na viwango vya kisekta/kiutaalamu katika kazi kama hizi.
- Usajili na leseni stahiki kutoka kwenye mamlaka za hapa nchini kwa ajili ya kutoa huduma hizo.

  - Uthibitisho wa usajili katika Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na Cheti cha Mwaka wa Karibuni cha Malipo ya Kodi.

Makampuni yenye nia, uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com (ukubwa usiozidi MB20)** kichwa cha habari kikiwa ni kumbukumbu namba husika hadi kufikia saa **11:00 jioni Majira ya Afrika Mashariki,** tarehe **21 Septemba 2021.**

**Muhimu: Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya makampuni ya Awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA).**

216462701

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kipaumbele kielekezwe kwenye kilimo cha ufuta

**ZAO** la ufuta linalimwa kwa wingi katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma, Pwani, Morogoro, Dodoma, Tanga na ukanda wa chini katika mikoa ya Rukwa na Mbeya kwa ajili ya chakula na biashara.

Kuna kampuni mbalimbali ambazo hununua ufuta kwa ajili ya soko la ndani na nyingine husafirisha zao hilo kwenda kuuza nje ya nchi, hali inayoonyesha kuwa kilimo cha ufuta kinalipa.

Mfano mzuri ni wa wakulima wa zao hilo Lindi ambao wamepata Sh. bilioni 120.6 baada ya kuuza kilo 49,885,228 za zao hilo kupitia mfumo wa stakabadhi gharani katika msimu wa mwaka huu.

Takwimu hizo ni za Mshauri wa Kilimo na Rasilimali Watu, Majid Myao, wakati akiwasilisha taarifa ya mauzo ya zao hilo katika mkutano uliowakutanisha wadau wa zao hilo.

Kwamba, Mkoa wa Lindi uliweka malengo ya kuzalisha kilo 68,500,000 za ufuta, lakini kutokana na hali ya hewa kutokuwa mzuri na idadi ya ukubwa wa mashamba wamekusanya kilo 49,885,228 sawa na asilimia 72.8, hivyo kushindwa kufikia lengo lililokusudiwa.

Hatua ya wakulima kupata kiasi hicho cha fedha katika mazingira hayo, ni wazi kwamba ipo haja kwa serikali kuweka mkazi kwenye kilimo cha ufuta, ili wakulima waweze kunufaika huku serikali nayo ikipata kodi.

Mbali na serikali kuliwekea mkazo zao hilo kwa kuhamasisha wakulima kujikita katka kulizalisha, pia serikali hainabudi kuweka mazingira mazuri na wezeshi kama kichocheo na hamasa.

Tunaamini kwamba kwa kilimo cha ufuta, wakulima wanaweza kuwa na maisha mazuri kwa kujenga nyumba bora, kusomesha watoto wao na hata kujiwekea akiba ya kutosha.

Kwa muda mrefu tumekuwa tukishuhudia wakulima hasa wa mikoa ya Kusini ya Lindi na Mtwara wakiweka nguvu zao zaidi kwenye kilimo cha zao la korosho ambalo wakati mwingine soko lake halina uhakika kutokana na wakati mwingine huporomoka.

Hivyo, kwa jinsi ambavyo ufuta umeanza kunufaisha wakulima, tunaona kuna haja wakahamasishwa kuongeza kasi katika kilimo cha ufuta ambacho nacho kimeanza kuonyesha wazi kuwa kinaweza kuwanufaisha.

Hatusemi kwamba, waache korosho, bali kasi inayotumika katika kilimo cha zao, iwe ni hiyo pia kwenye ufuta, ili kuboresha zaidi maisha yao, kutokana na kwamba nalo lina soko kama yalivyo mazao mengine na chakula na biashara.

Tunatambua kutegemea zao moja kwa ajili ya biashara, ni vigumu mkulima kufikia hatua nzuri ya maendeleo, bali kulima mazao mengi inaweza kuwa njia rahisi na mbadala kujiongezea kipato kupitia kilimo.


Wakati tunashauri serikali kuweka mkazo kwenye kilimo cha ufuta, si vibaya wakulima wenyewe nao wakajiongeza kwa kutambua umuhimu wa zao hilo na kuamua kuelekeza nguvu zao hilo.

Ufuta hutoa mafuta yanayotumika katika mapishi mbalimbali ili kuongeza ladha na pia huleta nguvu na joto mwilini, na mbegu zake huchanganywa na vyakula kama mikate, keki, mboga na kadhalika.

Jambo lingine linalothibitisha umuhimu wa zao la ufuta, ni jitihada za sasa za serikali kuhimiza uzalishaji wa mazao mbadala kwa lengo la kukabiliana na uhaba wa mafuta ya kupikia, hali inayosababisha bei kupanda kila uchao.

Kwa mtazamo wetu ni kwamba, wakulima wakihamasishwa na kutambua thamani ya zao hilo, wanaweza kuongeza kasi ya kilimo chake na kuwa na mashamba mengi, ambayo uzalishaji wake utakuwa mkubwa kisha kuwainua na taifa kwa ujumla kiuchumi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Jamii iunge mkono kuelimisha wasichana

Na Sabato Kasika

**LINAPOZUNGUMZWA S**uala la kumkomboa mwanamke, elimu ni kigezo muhimu na ndiyo msingi wa maisha ya kila mtu bila kujali ni mwanamke au mwanaume.

Takwimu zilizowahi kutolewa na Rais Samia Suluhu Hassan, zinaonyesha kwamba, kati ya wanafunzi wote wa shule za msingi, asilimia 50.4 ni wasichana, huku idadi yao katika shule za sekondari wasichana ni asilimia 43.9.

Ni katika mkutano wake na baadhi ya wanawake, ambao ulifanyika hivi karibuni jijini Dodoma, anapoeleza kuwa kila mmoja kwa nafasi yake ahakikishe anaunga mkono juhudi za kuwakwamua.

Anasema, serikali imedhamiria kutatua kero zinazomkabili mtoto wa kike kwenye elimu ikiwamo ufaulu mdogo katika masomo ya sayansi na sasa serikali imetangaza mradi wa ujenzi wa shule maalum za bweni za sekondari.

Ujenzi huo ulipangwa kuanza Julai mwaka huu, kwa kila mkoa, ili kufundisha masomo ya sayansi kwa wasichana, pia serikali imekuwa ikiweka fedha katika mfuko wa elimu ya juu ili kuongeza idadi ya wasichana vyuoni.

Hata hivyo, bado lipo tatizo analotaja Rais kuwa, ni jamii kusuasua linapokuja suala la kutoa fedha kumlipia msichana ada ili kujiendeleza kielimu, hali inailazimu serikali kuongeza fedha katika Mfuko wa Elimu huo mwaka hadi mwaka.

Katika ufafanuzi wake, Rais anasema, kwa mwaka wa fedha 2020/21, mfuko ulipewa Sh. bilioni 464 wakati mwaka huu wa 2021/22 mfuko wa elimu, umeongezewa fedha hadi kufikia Sh. bilioni 500.

Ni wazi serikali imedhamiria kumwinua mtoto wa kike katika elimu, hivyo hata jamii inaweza kuwa na sehemu ya kufanya katika harakati hizo za ukombozi kielimu.

Kwa kuwa kiongozi wa nchi anasema, bado jamii inasuasua linapokuja suala la kutoa fedha kumlipia mtoto wa kike, ili kujiendeleza kielimu, ni wazi wazazi na walezi, kila mmoja ana sehemu ya kufanya.

Ikumbukwe kuwa hatua ya serikali kujenga sekondari maalum za wasichana kila mkoa zenye bweni, ni dalili za kutosha kuwa imedhamiria kuhakikisha wasichana wanasoma bila usumbufu wowote.

Kwa hatua hiyo, si vibaya jamii nayo ikashiriki kwa hali na mali katika kufanikisha lengo hilo la kumkomboa mtoto wa kike kielimu, ili aepukane na mambo ambayo yanaweza kumkwamisha.

Ninaamini kwamba, ujenzi wa shule kama hizo, unasaidia mtoto wa kike kupata fursa ya kusoma vizuri akiwa katika mazingira rafiki yanayomwepusha na vishawishi vinavyoweza kumfanya ashindwe kutimiza ndoto zake kielimu.

Miongoni mwa sababu ambazo zimewahi kutajwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa ni Pamoja na miundombinu isiyo rafiki kwa wanafunzi kuanzia uchache wa vyoo, uhaba wa maji na ukosefu wa mabweni.

Katika mlolongo huo, kuna suala la umbali wa kutoka kwenye makazi hadi shule au vyuoni, hali ambayo wakati mwingine wanaweza kukutana na vishawishi vinavyoweza kuwafanya wasitimize ndoto zao.

Hali hiyo inaelezwa kuwa inawaathiri zaidi wanafunzi wa kike na kusababisha kuwapo kwa idadi kubwa ya watoto wa kike wanaokatisha masomo kutokana ya wale wa kiume.

Wakati serikali ikiweka mikakati hiyo ya kumnyanyua mtoto wa kike kielimu, ingependeza pia kama wahusika watatambua na kuthamini kinachofanywa kwa ajili yao ili waweze kunufaika.

Serikali inasema kuwa inanyanyua wanawake huku ikitambua kuwa wanatoa mchango mkubwa kwenye shughuli za kimaendeleo pia idadi kubwa ya watu wote Tanzania.

Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya 2012 wanawake ni zaidi ya asilimia 51.04 ya Watanzania hivyo ustawi na maendeleo ni lazima yapewe kipaumbele.

# Utouh ataja kikwazo kwa wakaguzi wa ndani

Na Allan Isack, ARUSHA

ALIYEKUWA Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali(CAG), Ludovick Utouh, amesema bado kuna tatizo kubwa kwa viongozi wakuu wa mashirika ya umma na taasisi binafsi kuwaingilia wakaguzi wa ndani katika utekelezaji wa majukumu yao.

Alisema kuingiliwa kwa wakaguzi wa ndani katika majukumu yao kunapunguza ufanisi na utendaji kazi, kwa kuwa hawapo huru kuwajibika ipasavyo.

Utouh, aliyasema hayo jana jijini Arusha wakat, akitoa mada katika mkutano wa wakaguzi wa ndani wa Tanzania na baadhi ya wakaguzi kutoka nchi mbalimbali za Afrika, pamoja na wakuu wa taasisi za umma na binafsi, uliondaliwa na Taasisi ya Wakaguzi wa Ndani Tanzania (IIA).

Mkutano huo uliwakutanisha wajumbe zaidi ya 300, kuelekea mkutano wa nane wa taasisi hiyo utakaofunguliwa na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, Septemba 22, mwaka huu.

Alisema awali wakaguzi wa ndali walipaza sauti kulalamikia kuingiliwa katika majukumu yao na viongozi wao wakuu katika mashirika na taasisi zao.

"Hali ya sasa siwezi kusema kwamba imetengemaa bado, kwa sababu kama mtakumbuka CAG, alipotoa ripoti yake Aprili mwaka huu, kuna halmashauri zilipata hati chafu na likatoka tamko la kuchukuliwa hatua kwa wakaguzi wa ndani.

"Kwa sisi tunavyofahamu namna wakaguzi wa ndani wanavyofanya kazi tulisema tamko lile lilikuwa la bahati mbaya sana, kwa kuwa wakaguzi wa ndani wao wanashauri na hawana mamlaka ya kutekeleza yale wanayoelekezwa," alisema na kuongeza:

"Kwa hiyo watu wakuchukuliwa hatua kwa kupatikana kwa hati chafu ni maofisa masuhuli ambao ndio wana wajibu wa kutekeleza mapendekezo yanayotoka katika ukaguzi wa ndani." Katika hatua nyingine, alisema kuna umuhimu wa uwajibikaji katika mpango wa kuleta maendeleo kwa kuwa maendeleo duniani yanakwenda sambamba na uwajibikaji.

"Nilitoa mada inayohusu uhusiano wa uwajibikaji na maendeleo, niliangalia zaidi kwenye taaluma ya ukaguzi wa ndani na wanahusikaje kwa sababu nchi inalilia sana maendeleo na Watanzania wanataka kupata maendeleo."

Alisema mkutano huo umelenga kukumbushana na kuelimishana kwa kuangalia uwajibikaji ni kitu gani na maendeleo ni nini na vitu hivyo vina mahusiano pamoja na nafasi ya wakaguzi wa ndani katika kuleta maendaleo,

Mratibu wa mkutano huo, Zelia Njeza, alisema lengo kutoa elimu kwa wakuu wa taasisi za umma na mashirika pamoja na wajumbe wa bodi.

Alisema katika mkutano huo wamezungumzia suala la uwajibikaji na utawala bora kwa mashirika na taasisi hizo, kwa kuwa wanapotekeleza majukumu yao wahakikishe shughuli hizo zinafanywa kwa maslai ya taasisi hizo na Taifa kwa ujumla.

"Tunaweza kutoa elimu kwa hawa wakurugenzi wa bodi mbalimbali nchini kwa ajili ya kuwawezesha wanapokuwa wakitoa huduma yao kuhakikisha taasisi zinajiendesha vizuri kwa malengo yao na nchi kwa ujumla kufahamu ni vitu gani wanavyotakiwa kuviandaa.

Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya Biashara ya Dar es Salaam (DCB), Zawadi Nanyaro, alisema kupitia mkutano huo wamejifunza kusimamia kampuni, taasisi na mashirika na namna ya kukabiliana na viashiria vinavyoweza kujitokeza kazini ikiwamo kupata hasara na wizi unaoweza kujitokeza.



Katibu Tawala wa Wilaya ya Handeni mkoani Tanga, Mashaka Mgeta (kushoto), akisaidiana na Diwani wa Kata ya Kwenjugo wilayani humo, Twaha Mgaya, kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya shule shikizi ya Koloja juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# MP amsimamisha kazi ofisa manunuzi Karagwe

Na Restuta Damina, KARAGWE

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amemsimamisha Kazi Ofisa Manunuzi wa Wilaya ya Karagwe, Yesse Kasanda, kwa madai ya kufanya manunuzi ya vifaa visivyokuwa na ubora vya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Kijiji cha Nyakanongo, Kata ya Kayanya iliyogharimu zaidi ya Sh. bilioni 2.3 iliyojengwa chini ya kiwango.

Aidha, alielekeza kuwa ili kufanikisha ujenzi huo wahusika wanatakiwa kutumia gharama zao kurekebisha kasoro zilizojitokeza kwa kuwa majengo yanaonekana yako chini ya kiwango.

"Kwa hali hii ya ujenzi chini ya kiwango kutokana na vifaa vilivyonunuliwa bado sijaridhishwa na ujenzi huo, katika jengo la mama na mtoto imeonekana uchakavu wa vigae na milango ikiwa haijakamilika kutoa huduma za afya,"alisema na kuongeza;

"Mnunuzi akae pembeni wakati akisuburi uchunguzi utakaofanywa na mkoa, Katibu Tawala wa Mkoa kusimamia watumishi wake katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo."

"Wakati uchunguzi unaendelea kufanyika wahusika watumie garama zao kubandua vigae ambavyo vinaonekana havifai kwenye jengo hili," alielekeza.

Pia Waziri Mkuu Majaliwa alitembelea mradi wa ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi VETA (KDVTC) wenye thamani ya Sh. bilioni 4.6. Katika hatua nyingine, alisema fedha za mkulima wa zao la kahawa zinaishia kwenye Vyama vya Msingi kutokana na makato mengi, ambayo siyo muhimu na hayajaagizwa na wizara, na kwamba usharika upo kwa ajili ya kusaidia na siyo kuwaumiza.

Waziri Mkuu alitembelea kiwanda cha kuchakata kahawa Ngara wilayani Ngara mkoani Kagera na kueleza kuwa wenyeviti wa ushirika wanatakiwa kuangalia mkulima anatatizo gani na kuwa na mkakati wa kutatua na siyo vinginevyo.

Kwa mujibu wa Majaliwa, zao hilo kuna makato mengi ambayo aliyataja kuwa ni Sh.328 badala ya 200 na ikiwa ni ongezeko la Sh. 128 kwa kila kilo moja.

Alisema mkulima anauza kahawa Sh. 1,300 na kwamba ilitakiwa iongezeke Sh. 128 ili auze Sh. 1,428 katika kilo moja.

Waziri Mkuu aliagiza wizara kufanya marekebisho ya makato ya ada ya usafiri, usafirishaji fedha ambayo ni Sh. 12 kwa kilo, bima ya mazao, ushuru wa ghala, mizani ya kupima na riba ya mkopo.

# Wagombea 10 upinzani waenguliwa udiwani

Na Marco Maduhu, SHINYANGA

WAGOMBEA 10 kutoka vyama vya upinzani, wameenguliwa kuwania udiwani wa Kata ya Ndembezi Manispaa ya Shinyanga, kwa madai ya kukosa sifa.

Msimamizi wa uchaguzi huo mdogo wa Kata ya Ndembezi, Manispaa ya Shinyanga, Timothy Andrew, akizungumza jana na waandishi wa habari, alisema baadhi ya wagombea wa vyama hivyo vya upinzani, hawakukidhi vigezo vya kugombea udiwani, huku wengine wakishindwa kurudisha fomu.

Aliwataja wagombea walioenguliwa kuwa ni Abdala Sube kutoka Chama cha Demokrasia Makini, Rehema Mjengi (ACD), Antony Ndinda (SAU), Ramla Shija (NLD), Fatuma Ally (UMD), Emiliana Malema (CCK), Ibrahim Juma (CHAUMA), Lwitakubi Kabugulu (NRA), Amen Isangi (DP) na Mvano Idd, ACT-Wazalendo.

Pia alimtaja mgombea aliyekidhi vigezo vya Tume ya Taifa ya Uchaguzi na kupitishwa kugombea udiwani kata hiyo kuwa ni Victor Mmanywa kutoka CCM.

"Baada ya kikao kukaa na kumpitisha mgombea wa CCM, na kuwaengua wagombea wengine walikosa vigezo, kinachofuata ni zamu ya wananchi kuleta mapingamizi, ili tuendelee na hatua zingine za uchaguzi," alisema Andrew.

Sababu ya kuengeliwa mgombea wa ACT-Wazalendo aliyekuwa ameteuliwa rasmi na kupewa barua ya uteuzi imeelezwa kuwa hakujaza fomu namba 8 (c) na namba 10 (c) na kuzirudisha NEC kwa wakati.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu jana, Katibu Mwenezi wa chama hicho Jimbo la Shinyanga mjini, Omary Gindu, alisema mgombea wao alikuwa tayari amepewa barua ya uteuzi na kwamba mgombea wa CCM alimuwekeza pingamizi kwamba hakujaza fomu hizo kwa usahihi.

Kutokana na hatua hiyo, chama hicho kimesema kinajiandaa kukata rufani ngazi ya jimbo na nakala kuipeleka NEC ili kupata haki yao.

Naye mmoja wa wagombea udiwani ambaye ameenguliwa kwenye kinyang'anyiro hicho, Abdalla Sube, alikiri kuchelewa kurudisha fomu kwa maelezo kuwa gari alilokuwa amepanda akitokea Ushetu wilayani Kahama kuja Shinyanga mjini kupata matatizo njiani.

Uchaguzi huo mdogo katika Kata ya Ndembezi Manispaa ya Shinyanga, unafanyika kufuatia kifo cha aliyekuwa Diwani wa kata hiyo, David Nkulila, ambaye alikuwa Meya wa Manispaa ya Shinyanga, aliyefariki dunia Agosti, mwaka huu kwa maradhi ya moyo.

# Matukio 30 ukatili wafanya kazi nyumbani yaripotiwa

**Na Elizabeth Faustine,**

MWANZA

ZAIDI ya matukio 30 ya ukatili kwa wafanyakazi wa nyumbani yameripotiwa ndani ya mwezi mmoja katika wilaya tatu mkoani Mwanza.

Takwimu hizo zilitolewa mwishoni mwa wiki na Mratibu wa Taasisi ya Tanzania Child Domestic Workers, George Leonard, alipozungumza na Nipashe na kuzitaja wilaya hizo kuwa ni Ilemela, Nyamagana na Magu.

Alisema wafanyakazi wa kazi za ndani wanakabiliwa na tatizo la kutolipwa mishahara, kufanyishwa kazi zisizoendana na umri wao pamoja na kupewa lugha za matusi na kejeli.

"Ndani ya mwezi mmoja wa Agosti, mwaka huu kesi ambazo zimeripotiwa kwetu ni zaidi ya 30, ukienda ustawi wa jamii au dawati la jinsia polisi utazikuta, unaweza kukuta binti amefanya kazi miaka miwili au mmoja, lakini hajalipwa mshahara na wengine wanapojaribu kudai wanabambikiwa kesi na mambo yanazidi kuwa magumu zaidi," alisema Leonard.

Alitoa wito kwa jamii kutoa mchango wa kuwaelimisha ili kuondokana na vitendo vya ukatili kwa wafanyakazi na kuwafanya sehemu ya familia zao.

"Kila mmoja wetu ajaribu kutoa mchango wake kwa maana ya viongozi wa serikali za mitaa, waandishi wa habari, mashirika yanayotetea haki za watoto, wadau pamoja na wanaharakati wengine ambao wanapinga vitendo vya ukatili kwa watoto ili kuondoa vitendo vya ukatili kwa watoto," alisema Leonard.

Aliwataka wazazi kuhakikisha wanawapatia watoto wao haki zao za msingi kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 ikiwamo kuwapa watoto haki ya kupata elimu.

"Kuna watoto ambao wameingia kwenye ajira ambao hata darasa la saba hawajamaliza, hivyo ni wajibu wa mzazi kuhakikisha kuwa tunawalinda watoto na kuwapatia elimu stahiki ikayowawezesha kumudu maisha," alisema.

Alisema zaidi ya asilimia 80 ya watoto wanaopata ajira ni wa kike, waajiri wanapaswa kuzingatia suala la afya, pia kufuata sheria na taratibu ikiwamo kuzingatia suala la umri wa mtoto.



Mkuu wa Idara ya Ufanisi wa Kampuni ya Vodacom Tanzania Plc, Sorayya Shareef, akimkabidhi cheti mmoja wa wasichana waliohudhuria mafunzo ya TEHAMA yaliyopewa jina la 'Code like a girl', mpango unaoendeshwa na kampuni hiyo, kupitia Taasisi ya dLab, ili kuhamasisha wasichana kupenda masomo ya sayansi, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Mkuu wa Idara ya Sayansi na Utafiti kutoka dLab, Mahadia Tunga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Polisi kukomesha uhalifu Ziwa Victoria

**Na Richard Makore,** MWANZA

JESHI la Polisi limeahidi kukomesha na kupambana na wahalifu katika Ziwa Victoria ili kuwapa fursa wavuvi kufanya shughuli zao na kukuza uchumi.

Azimio hilo lilitolewa jana jijini hapa na Kamishina wa operesheni na mafunzo wa jeshi hilo kutoka makao makuu, Lebaratus Sabas, alipofungua kikao kazi kilichowashirikisha makamanda wa polisi na wapelelezi wa mikoa, wakuu wa polisi wa wilaya, wavuvi, maofisa uvuvi pamoja na wadau wa uvuvi katika ziwa hilo.

Wadaau hao wanaotoka mikoa sita ya Kanda ya Ziwa ikiwamo, Mwanza, Geita, Kagera, Tarime/Rorya, Simiyu na Mara na wamekutana kwa ajili ya kujadili namna ya kumaliza uhalifu katika ziwa hilo.

Alisema kwa sasa matukio ya uhalifu yamepungua katika ziwa hilo, lakini anataka kuona yanaisha ili wananchi waweze kufanya shughuli zao vizuri.

Alisema lengo la kikao hicho ni kuhakikisha wanashirikiana na wadau wengine ili waweze kupata taarifa nyingi za uhalifu na kuzishughulikia.

Akizungumza katika kikao hicho kabla ya kumkaribisha, Kamishna Sabas, Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Mwanza, Ramadhan Ng'anzi alisema, suala la usalama katika ziwa hili ni la wadau wote.

Alisema uhalifu hauchagui bali mtu yeyote anaweza kufanyiwa uhalifu na ili kuukomesha wadau wote wanatakiwa kushiriki.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kufunguliwa kikao hicho, Mwenyekiti wa Chama cha Wavuvi Nchini (TAFU), Bakari Kadabi, alisema uhalifu umejikita katika maeneo ya visiwani.

Alisema wengi hukimbilia huko na kujificha ili waendelee kufanya uhalifu na kwamba nguvu ya pamoja na vyombo hivyo itasaidia kumaliza tatizo hilo.

# Kituo chaibua watoto 84 wenye ulemavu waliofichwa

**Na Christina Haule,**

MOROGORO

KITUO Cha watoto wenye ulemavu wa akili na viungo (Amani Center) cha mjini hapa kimefanikiwa kuibua watoto 84 wenye ulemavu waliofichwa majumbani katika kipindi cha mwaka 2020/21.

Watoto hao wameibuliwa kutoka kwenye vijiji mbalimbali mkoani hapa, huku 12 kati yao wakitarajia kupelekwa Hospitali ya CCBRT kwa ajili ya upasuaji.

Mkurugenzi wa Kituo cha Amani, Padre Beatus Sewando, alisema jana kuwa watoto hao 84 wameibuliwa kutoka katika vijiji vya Matombo, Kiroka, Mandela mkoani Pwani, Chakwale na Magubike wilayani Gairo, Dakawa na Lumbiji, wilayani Kilosa.

Alisema mwaka 2020 kituo hicho kilianza utaratibu wa kutembelea vijiji vya wilaya mbalimbali mkoani hapa na kuibua watoto hao baada ya kufanya utafiti na kubaini kuwa licha ya elimu inayoendelea kutolewa kwa jamii nchini bado kuna watu wanaendekeza dhana ya kuwaficha watoto hao ndani. Padre Sewando alisema watoto 17 waliibuliwa mwaka 2020 na wote wameshafanyiwa upasuaji na hali zao zinaendelea vizuri ambapo mwaka 2021 wameibua jumla ya watoto 67 na 12 kati yao wanatarajia kupelekwa kwenye upasuaji katika Hospitali ya Rufani Muhimbili kitengo cha CCBRT kwa ajili ya upasuaji.

Alisema watoto hao wameibuliwa baada ya kituo hicho kuwa na utaratibu wa kutembelea vijiji kuibua watoto wenye ulemavu, kutoa elimu na kusaidia wengine kimatibabu na mazoezi.

Aliwaomba wenyeviti wa vijiji kuendelea kutoa ushirikiano katika kuwaibua watoto hao na viongozi wa dini kuendelea kutoa elimu baada ya ibada juu ya umuhimu wa kumthamini mtoto mwenye ulemavu kwa sababu ni sawa na mtoto mwingine asiye na ulemavu anayestahili kupata haki zake zote.

Alisema wamebaini suala la ukosefu wa imani kutoka kwa wazazi kuwa watoto wanaweza kupona linachangia watoto hao kuendelea kufichwa na kukosa kupewa matibabu mapema hali inayoweza kusababisha wengine kushindwa kupona hata kama walikuwa na uwezekano wa kupona.

"Utakuta mtoto yupo chini kabisa na umri wake unazidi kusogea na ukimwangalia alikuwa na uwezo wa kuinua kabisa kama angepatiwa tiba na mazoezi kwa wakati," alisema Padre Sewando.

Naye mmoja wa watoto waliopata matibabu na mazoezi katika kituo hicho na kupata nafuu, Romayana Mdalo, alikishukuru kituo hicho kwa kumsaidia kutembea.

Kituo hicho cha Amani Center chenye kulea watoto wenye ulemavu na akili kilianzishwa mwaka 1992 kikiwa na jumla ya watoto saba mpaka sasa kina 135 huku wengi wao wakiwa wametelekezwa na wazazi wao na wengine yatima.

## Mgodi kusaidia huduma za kijamii kwa mil. 300/-

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MGODI wa Dhahabu wa Buckreef Mkoa wa Geita imetenga zaidi ya Sh. milioni 300 kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wa mkoa huo kwa sekta ya elimu, kuchimba visima vya maji pamoja na afya.

Akizungumza na waandishi wa habari kwenye maonyesho ya nne ya teknolojia na uwekezaji kwenye sekta ya madini Mkoa wa Geita, Meneja wa Rasilimali Watu wa mgodi huo, Amelda Msuya, alisema lengo la Buckreef ni kuhakikisha jamii inayozanguka mgodi huo inanufaika.

Msuya alisema tangu Buckreef ianze imejenga madarasa manne katika Shule ya Msingi Tembo iliyopo Kata ya Kaseme Wilaya ya Geita pamoja na msaada wa madawati 300 yenye uwezo wa kukalia wanafunzi 600 katika Shule ya Sekondari Kaseme.

Aidha, alisema Buckreef kwa kushirikiana na TARURA imerekebisha barabara ya Katoro- Lwamgasa kwa kuweka mawe na moramu ili kuhakikisha inapitika kwa urahisi.

Alisema Mgodi wa Buckreef unakamilisha mchakato wa fidia kwa wananchi 960 wanaozunguka mgodi huo ambalo una kilomita 9.6 kwa kuwalipa Sh. bilioni 6.

Msuya alisema mgodi wa Buckreef unatarajia kujenga madarasa mawili katika Shule ya Sekondari Lwamgasa pamoja na matundu ya choo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Aidha, alisema Mgodi wa Buckreef umejipanga kuhakikisha unaongeza madarasa katika Shule ya Sekondari Busanda iliyoko Wilaya ya Geita.

Alisema Buckreef inatarajia kujenga Kituo cha Afya Bugulula kilichoko Halmashauri ya Mji Geita ili wananchi wapate huduma kwa karibu.

## Shule yapigwa jeki meza, viti

**Na Sabato Kasika**

SHULE ya Sekondari Utete, iliyopo Wilaya ya Rufiji mkoani Pwani, imepata msaada wa viti, 50 na meza 50, ambavyo vimetolewa na Benki ya NMB vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 4.5.

Msaada huo ulikabidhiwa juzi na Kaimu Meneja wa NMB Kanda ya Mashariki, Harold Haule Lambilaki, huku akifafanua kuwa umetokana na faida ambayo benki hiyo hupata na kurejesha kwa jamii katika miradi ya elimu na afya.

"NMB tumeshatoa misaada yenye thamani ya Sh. bilioni 8 yakiwamo magodoro na vitanda na magodoro katika hospitali za vijijini na tumesaidia katika mjanga mbalimbali," alisema Lambaliki.

Akizungumza baada ya kupokea msaada huo, Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Meja Edward Gowelo, aliishukuru benki hiyo kutoa viti na meza kwa shule hiyo na kuwataka wanafunzi na uongozi wa shule kuvitunza.

"Rai yangu kwenu wanafunzi na uongozi wa shule ni kutunza vizuri vitu hivi, ili hata wanafunzi watakaochaguliwa kujiunga na shule hii baadaye, wavitumie," alisema Meja Gowelo.

Mkuu wa shule hiyo, Bassa Ngela, alisema, inakabiliwa na tatizo la uchakavu wa majengo, bwalo la kulia chakula kwa wanafunzi na upungufu wa vitanda ambapo ameomba wadau mbalimbali kuwasaidia kutatua tatizo hilo.

"Shule hii ilianzishwa mwaka 1940 wakati huo ikiwa ni ya msingi, lakini baadaye mwaka 1990, ilibadilishwa na kuwa ya sekondari na kwamba, kwa sasa ina wanafunzi 1361," alisema Ngella.

Aliishukuru Benki ya NMB kwa msaada huo na kuahidi kuwa vitatunzwa na kwamba vimepatikana kwa wakati mwafaka, kwa kuwa shule hiyo pia ina uhaba wa viti na meza.

# Watendaji wapewa mwezi kukamilisha wodi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SONGWE

WATENDAJI katika Halmashauri ya Wilaya ya Ileje, mkoani Songwe wametakiwa kufanya kazi usiku na mchana kukamilisha ujenzi wa wodi tatu za watoto, wanawake na wanaume.

Ujenzi huo ni sehemu ya upanuzi wa Hospitali ya Wilaya ili zianze kutoa huduma zilizokusudiwa kwa wananchi.

Maelekezo hayo yalitolewa juzi na kiongozi wa mbio za Mwenge Taifa, Luteni Josephine Mwambashi, baada ya kukagua na kuweka jiwe la msingi katika mradi huo unaojengwa kwa mfumo wa nguvu za wananchi (force account) ambapo serikali imetoa shilingi milioni 500 na mchango wa wananchi ukiwa shilingi 650,000.

"Kwa sababu kwenye taarifa yenu mliotusomea kuwa mradi utakamilika Oktoba, pia tumekwenda kwenye stoo kuangalia baadhi ya vifaa vilivyopo na kulinganisha na fedha zilizotumika, fanyeni kazi usiku na mchana ili mwezi Oktoba wananchi waanze kupata huduma kwa kuwa vifaa vipo," alisema Luteni Mwambashi.

"Tunaishukuru serikali yetu kwa kuona umuhimu kwa kutuletea fedha kwa ajili ya ujenzi wa wodi hizi tatu, kinachobaki kwetu ni wale tunaopewa dhamana ya kusimamia kutanguliza uzalendo na haki ili kutimiza malengo ya kutoa huduma kwa wananchi," aliongeza Mwambashi.

Akisoma taarifa ya ujenzi wa wodi hizo tatu kwa kiongozi wa mbio za Mwenge, Kaimu Mganga Mkuu wa Hospitali ya Wilaya ya Itumba, Michael Mwita, alisema lengo la mradi huo wenye thamani ya shilingi 500,650,000 ni kuboresha mazingira ya kutolea huduma za afya kwa jamii.

"Kukamilika kwa mradi huu kutawezesha utoaji huduma bora za afya kwa wilaya kwa takribani wakazi 160,000 wanategemea kupata huduma kutoka kwenye hospitali hii pamoja na maeneo jirani," alisema Dk. Mwita.

Mkuu wa Wilaya ya Ileje, Anna Gidarya, alisema maagizo yote yaliyotolewa na kiongozi wa mbio za Mwenge kitaifa watayafanyia kazi ili kuhakikisha wananchi wanaanza kupata huduma muhimu ambazo wamezisubiri muda mrefu.



Meneja Mkuu wa kampuni ya umma inayotoa elimu ya kilimo chenye tija, masoko ya uhakika ya mazao mbalimbali na mikopo isiyokuwa na riba kwa wakulima wadogo ya JATU PLC, Mohamed Issa Simbano (kulia), akizungumza na wakulima mbalimbali waliojitokeza katika Viwanja vya Uhuru Park mijini Moshi juzi, wakati wa Maonyesho ya Wiki ya Kilimo Kanda ya Kaskazini yanayoendelea mjini hapo kwa kuratibitiwa na kampuni hiyo. **PICHA: JAMES LANKA**

# Wafugaji waonyeshwa fursa ya mifugo

**Na Mbaraka Kambona,** RUFIJI

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amewataka wafugaji wa Mkoa wa Pwani kuanza kuvuna mifugo yao na kuiuza, kwani kwa kufanya hivyo kutawasaidia kuwaongezea kipato na kupunguza migogoro kati yao na watumiaji wengine wa ardhi.

Ulega aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza na wafugaji na wakulima wa Wilaya ya Rufiji alipofanya ziara ya kusikiliza kero zao na kuzitafutia ufumbuzi.

Alisema ni muhimu viongozi wa wilaya za Rufiji, Mkuranga na Kibiti kukaa na wadau wa mifugo kutengeneza mkakati wa kuhamasisha uvunaji wa mifugo yao kwa kuwa soko la kuuza lipo mkoani humo na bado hawajalitumia ipasavyo.

"Hapa Mkoa wa Pwani tuna Kiwanda cha Nyama cha Tan-Choice, lakini pamoja na kiwanda hicho kuwapo hakuna mifugo inayopelekwa pale kutoka ukanda wetu huu wa Pwani," alisema Ulega.

Aliongeza kuwa ili faida ya uwapo wa kiwanda hicho ionekane, hivyo ni vyema wadau wote wa mifugo mkoani humo waanze uvunaji mkubwa na kupeleka kuiuza kiwandani hapo.

"Tunatamani kuona mifugo inatoka katika ukanda huu wa Pwani na kwenda kuuzwa jijini Dar es Salaam ambapo ndipo kwenye biashara kubwa ya nyama, msione fahari kukaa na makundi makubwa ya mifugo ambayo mwisho wa siku yakaonekana kuwa ni kero na hayana faida," aliongeza Ulega.

Kuhusu kuboresha huduma za mifugo, Waziri Ulega alisema kuwa katika Bajeti ya Mwaka huu 2021/ 2022 serikali imepanga kununua pikipiki 300 na itazigawa kwa maofisa ugani nchi nzima, ili waweze kutoa huduma ya mifugo kwa ufanisi.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Meja Edward Gowelle, alisema kufuatia migogoro mingi iliyoibuka, ameanzisha sensa ya mifugo na wafugaji ili kujua idadi yao halisi na kupanga mipango ya matumizi bora ya ardhi kulingana na mahitaji.

# Asilimia 85 sekta isiyo rasmi ni wanagenzi

**Na Christina Mwakangale**

ASILIMIA 85 ya Watanzania waliojiajiri katika shughuli zisizo rasmi ni wanagenzi wakirithi mafunzo kutoka kwa wazazi, walezi wao huku vikwazo vikuu ikiwa ni namna ya kuboresha mbinu za uanagenzi.

Ofisa Mawasiliano wa Progamu za Ujuzi kutoka Shirika la Kazi Duniani (ILO), Belinda Japhet, aliyasema hayo ijini Dar es Salaam kwa waandishi wa habari kuhusu namna ya kuzingatia uandishi bora unaozingatia ujuzi.

Alisema kupitia Progamu ya ujifunzaji wa ngazi ya awali (RPL), inayoratibiwa na ILO, lengo ni kuwafikia, kuwatambua wanagenzi waliopata ujuzi wa shughuli zao kutoka kwenye familia na kuwapatia mafunzo rasmi na kisha kuwapatia vyeti.

"Kwa bahati mbaya wanagenzi ambao ni kati ya Watanzania wengi, hawatambuliwi rasmi na taasisi za mafunzo. RPL programu ambayo inatambuliwa na serikali ya Tanzania, unaruhusu kuwafunza wasio kwenye mfumo rasmi kujifunza na kupata vyeti kutoka Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA).

"Programu hii ni ya kipekee inaweka msisitizo katika kuidhinisha ujifunzaji wa mapema, ambayo ni maarifa au ujuzi uliopatikana katika masomo na uufanyie kazi kupitia uzoefu. RPL inazingatia matokeo ya ujifunzaji na sio jinsi ujuzi umepatikana," alisema Belinda.

Kuhusu programu hiyo, Belinda alibainisha ni mpango ulio wa pamoja kati ya ILO na Ofisi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama ili kuendeleza ujuzi.

Belinda alisema programu hiyo inawaanda wanagenzi hususan vijana ambao ni nguvukazi, kujiunga kwenye mageuzi ya kiuchumi katika jamii na kukamilisha matokeo ya uchumi wa kati 2025 na kwamba mafanikio yameonekana Zanzibar, katika utafiti uliofanywa mwaka 2019.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, akizungumzia programu hiyo, alibainisha kwamba ni muda wa Watanzania ambao hawajapata ujuzi rasmi kujiunga na mpango huo.

"Tunatoa wito kwa vijana ambao wana ujuzi katika kufanya shughuli zao, lakini hawana vyeti, wajiunge na RPL kupitia vyuo vya VETA ili kupata mafunzo," alisema Mhagama.



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega akiongea na wafugaji, wakulima wa Wilaya ya Rufiji (hawapo pichani), alipofanya ziara wilayani humo kwa lengo la kusikiliza kero na kuzitatua. Kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Meja Edward Gowelle. **PICHA: MBARAKA KAMBONA**

# Viongozi wa dini wafunguka Siku ya Amani

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKATI leo dunia inaadhimisha Siku ya Amani, viongozi kadhaa wa dini wamefunguka kuhusiana na suala la amani.

Katika maadhimisho hayo leo jijini Dodoma, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi.

Siku ya Amani Kimataifa huadhimishwa na nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa (UN) kila mwaka Septemba 21, ambapo hutumia siku hiyo kukutanisha wadau mbalimbali kufanya mijadala inayohusu amani.

Ofisa Habari wa Umoja wa Mataifa (UN) nchini, Stella Vuzo, alisema maadhimisho hayo yatafanyika katika ukumbi wa Chuo cha Mipango.

Alisema maadhimisho hayo yatatanguliwa na shughuli mbalimbali ambazo watazifanya ikiwamo kupanda miti.

"Katika siku hii mapigano yote yatasitishwa kwa saa 24, nchi ambazo zinapigana zinatakiwa kuangalia dunia inakuwa sehemu salama ya kuishi," alisema.

Aidha, Vuzo alisema kauli mbiu ya mwaka huu ni kujikwamua zaidi katika dunia yenye usawa zaidi, kwani dunia imekumbwa na changamoto ya Uviko-19, lakini inatakiwa kutafakari ni jinsi gani itajikwamua katika changamato hiyo.

"Tutakuwa na wawakilishi kutoka serikalini, mwakilishi mkazi Tanzania wa UN, viongozi mbalimbali wa dini, vijana asasi mbalimbali ambao wote kwa pamoja watazungumzia jinsi yakudumisha amani," alisema Vuzo

Aidha, alisema siku hii itatanguliwa na shughuli mbalimbali za kijamii ambapo watatembelea Shule ya Sekondari Kikuyu na Chinangali pamoja na kupanda miti.

Askofu wa Kanisa la Menonite Kanda ya Kati, Joseph Mutolela, alisema kuwa mwasisi wa amani ni Yesu Kristo kwani alihubiri na kuwataka watu wawe na amani na watu wote.

"Kupitia maadhimisho haya niwatake Watanzania waendelee kuienzi amani waliyoiacha waasisi wa hii, wao kama viongozi wa dini wataendelea kukemea uovu na kuhubiri amani," alisema askofu huyo.

Shekhe Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mustafa Shaban, alisema suala la amani lipo hata katika vitabu vyote vya dini, kwani hata mitume walitaja kuna nyumba ya amani.

"Suala la amani ni suala ambalo Mwenyezi Mungu aliwataka watu wote wazingatie amani, licha ya kuwa kuna magonjwa makubwa kama Tauni lakini hakuacha kuhubiri amani," alisema Shekhe huyo.

## Watendaji wapewa jukumu la viwango bidhaa wajasiriamali

**Na Mwandishi Wetu,** LINDI

WATENDAJI katika halmashauri zote za Mkoa wa Lindi, wametakiwa kuendelea kutoa ushirikiano kwa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ili liweze kutimiza azma yake ya kuhakikisha wajasiriamali wanaosindika korosho na bidhaa zake wazalishe bidhaa zinazokidhi viwango.

Wito huo ulitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Zainab Terack, wakati akifungua mafunzo ya wajasiriamali ambao ni wasindikaji wa wafungashaji wa bidhaa za korosho yaliyofanyika mkoani hapa.

Alisema baada ya mafunzo hayo kutakuwa na fursa wa washiriki ambao watakuwa tayari kutembelewa na maofisa wa shirika hilo kupewa mafunzo na ushauri katika maeneo yao ya usindikaji.

Alisema ni muhimu kwa watendaji kwenye halmashauri zote za mkoa huo kutoa ushirikiano kwa maofisa hao wa TBS.

"Uongozi wa mkoa unaamini mafunzo haya ni njia muafaka ya kuleta tija zaidi katika juhudi za kuliletea taifa letu maendeleo ya haraka kulingana na fursa zilizopo hasa kwenye sekta ya viwanda, kilimo, biashara na maeneo mengine mengi," alisema Terack na kuongeza:

"Mafunzo haya yamekuja kwa wakati mwafaka ambapo serikali imeazimia kwa dhati kabisa kuendeleza viwanda ili kutoa ajira katika kada mbalimbali pamoja na kuziwezesha bidhaa zetu kushindana katika masoko ya ndani, kikanda na nje ya Tanzania," alisema.

Alifafanua kuwa mafunzo hayo ni uthibitisho wa azma ya serikali kupitia taasisi zake katika kufanikisha malengo ya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati kupitia uwekezaji katika viwanda.

Kwa upande wake uongozi wa Wilaya ya Nachingwea ulisema mafunzo hayo yatakuwa ni nyenzo muhimu kwa wajasiriamali na watakwenda kufanikisha malengo ya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati kupitia uwekezaji katika viwanda.

Akifungua mafunzo ya aina hiyo yaliyofanyika mwishoni mwa wiki wilayani humo kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya, Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya ya Nachingwea, Lilian Mwaipungwa, alisema hatua hiyo italiongezea Taifa fedha za kigeni kupitia zao la korosho.

Meneja wa Utafiti na Mafunzo TBS, Hamisi Sudi Mwanasala, aliuhakikishia uongozi wa Wilaya ya Nachingwea kwamba shirika hilo limepania kuhakikisha bidhaa zitokanazo na korosho zinazalishwa kwa kuzingatia ubora wa viwango vinavyokubalika katika soko la nje kwa kuwapatia mafunzo ya kutosha wajasiriamali.

**"Mafunzo haya yamekuja kwa wakati mwafaka ambapo serikali imeazimia kwa dhati kabisa kuendeleza viwanda ili kutoa ajira katika kada mbalimbali pamoja na kuziwezesha bidhaa zetu kushindana katika masoko ya ndani, kikanda na nje ya Tanzania," alisema.**

# TANGAZO

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## WIZARA YA MAJI

## TANGAZO LA NAFASI YA MWENYEKITI WA BODI YA MAJI YA TAIFA

Katibu Mkuu, Wizara ya Maji anatangaza nafasi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Maji ya Taifa. Bodi hii inaundwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka 2009 chini ya Kifungu Na. 20. Muda wa Bodi ni miaka mitatu.

**MAJUKUMU YA BODI YA MAJI YA TAIFA**

(a) Kuchunguza jambo lolote litakalowasilishwa kwake na Waziri au Wizara ya Sekta nyingine kuhusiana na usimamizi endelevu wa rasilimali za maji na kutoa mapendekezo yao kwa Waziri au Wizara ya Sekta husika, itakavyoona inafaa, kuchukua hatua madhubuti ili kufikia malengo ya Sheria hii;
(b) Kushauri vipaumbele vya uwekezaji na mpangilio wa kifedha na kuratibu na kuunganisha miradi inayotekelezwa kwa fedha za nje na programu zenye kutoa mchango wa kuendeleza rasilimali za maji;
(c) Kushauri katika kujumuisha mipango ya sekta mbalimbali kuhusu tathmini na kupanga rasilimali za maji;
(d) Kushauri uratibu wa mipango ya bonde na usimamizi;
(e) kushauri utatuzi wa migogoro kati ya sekta moja na nyingine na kati ya Bonde moja na lingine;
(f) Kushauri vipaumbele vya uwekezaji na mpangilio wa kifedha;
(g) Kushauri uhamisho wa maji baina ya mabonde;
(h) Kushauri usimamizi wa rasilimali za maji shirikishi,
(i) kupendekeza kwa Waziri hatua za kisheria kwa ajili ya usimamizi wa rasilimali za maji na njia madhubuti ya kuzuia uchafuzi wa maji;
(j) Kushirikiana na Mkurugenzi kwenye masuala ya kiufundi;
(k) Kuandaa taarifa ya kila nusu mwaka ya hali ya rasilimali za maji; na
(l) Kutekeleza majukumu mengine ya kiushauri ya Sekta kama Waziri atakavyoona inafaa.

**SIFA ZA MWOMBAJI**
Mwombaji wa nafasi hii anatakiwa kuwa na ujuzi na uzoefu katika masuala ya Sekta ya Maji au Sekta zinazohusiana na sekta hiyo. Awe na uzoefu na ujuzi katika masuala ya uongozi na usimamizi katika nyanja zinazohusiana na masuala ya usimamizi wa rasilimali za maji kwa muda usiopungua miaka 10. Aidha, awe na ujuzi mahsusi kwenye masuala ya usimamizi wa rasilimali za maji na asiwe/ asitoke kwenye taasisi ambayo ni mtumiaji mkuu wa maji (Major Water User).

**Maombi yatumwe kwa:**

**Katibu Mkuu,**
**Wizara ya Maji,**
**Mji wa Serikali,**
**Mtaa wa Maji,**
**S.L.P. 456,**
**40473, DODOMA.**

Nakala ya maombi itumwe kupitia barua pepe: **ps@maji.go.tz**

Maombi yaambatishwe na wasifu wa mwombaji (CV) yenye wadhamini watatu na namba zao za simu. Andika **"Mwenyekiti Bodi ya Maji ya Taifa"** nyuma ya bahasha. Mwisho wa kupokea maombi ni siku ya Ijumaa tarehe 15 Oktoba, 2021 saa 09.30 alasiri

**Imetolewana:**

**Katibu Mkuu**
**Wizara ya Maji**
**17 Septemba, 2021**

216468302

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## WIZARA YA MAJI

## TANGAZO LA NAFASI YA MWENYEKITI WA BODI YA MAJI YA BONDE LA ZIWA VICTORIA

Katibu Mkuu, Wizara ya Maji anatangaza nafasi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Victoria. Bodi hii inaundwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka 2009 chini ya Kifungu Na. 22. Muda wa Bodi ni miaka mitatu.

**MAJUKUMU YA BODI YA MAJI YA BONDE LA ZIWA VICTORIA**

(a) Kuandaa mipango ya usimamizi wa rasilimali za maji, miradi, bajeti na mkakati wa utekelezaji wa Bonde;
(b) Kuunganisha mipango ya Wilaya kwenye mipango ya usimamizi wa rasilimali za maji ya Bonde;
(c) Kutoa miongozo na viwango vya ujenzi na matengenezo wa miundombinu ya vyanzo vya maji;
(d) Kufuatilia, kutathmini na kuidhinisha ujenzi na matengenezo wa miundombinu ya vyanzo vya maji;
(e) Kukusanya, kuchakata na kuchambua takwimu zinazohusu usimamizi wa rasilimali za maji;
(f) Kutunza na kuboresha tathmini za upatikanaji mahitaji ya rasilimali za maji;
(g) Kuidhinisha, kutoa na kufuta vibali vya kutumia maji na kutiririsha majitaka;
(h) Kutunza Daftari la Maji kulingana na Kifungu cha 78;
(i) Kufuatilia na kutekeleza vibali vya kutumia na kutiririsha majitaka na hatua za kuzuia uchafuzi;
(j) Kutatua migogoro ndani ya Bonde;
(k) Kutekeleza miradi na programu za usimamizi wa rasilimali za maji;
(l) Kuratibu shughuli za kisekta za usimamizi wa rasilimali za maji katika ngazi ya bonde na kuwa kiungo cha mawasiliano kati ya Sekta na watumiaji wa maji kwa ujumla;
(m) Kumshauri Mkurugenzi kwenye mambo ya kiufundi yanayohusu masuala ya maji shirikishi katika bonde;
(n) Kuteuwa Mwenyekiti na wajumbe wa kamati za dakio na kidakio maji; na
(o) Kutayarisha taarifa juu ya hali ya rasilimali za maji katika Bonde.

**SIFA ZA MWOMBAJI**
Mwombaji wa nafasi hii anatakiwa kuwa na ujuzi na uzoefu katika masuala ya Sekta ya Maji au Sekta zinazohusiana na sekta hiyo. Aidha, awe na ujuzi mahsusi kwenye masuala ya usimamizi wa rasilimali za maji na asiwe/ asitoke kwenye taasisi ambayo ni mtumiaji mkuu wa maji (Major Water User).

Maombi yatumwe kwa :

**Katibu Mkuu,**
**Wizara ya Maji,**
**Mji wa Serikali,**
**Mtaa wa Maji,**
**S.L.P. 456,**
**40473, DODOMA.**

Nakala ya maombi itumwe kupitia barua pepe: **ps@maji.go.tz**

Maombi yaambatishwe na wasifu wa mwombaji (CV) yenye wadhamini watatu na namba zao za simu. Andika **"Mwenyekiti Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria"** nyuma ya bahasha.

Mwisho wa kupokea maombi ni siku ya Ijumaa tarehe **15 Oktoba, 2021 saa 09.30 alasiri**

**Imetolewana:**

**Katibu Mkuu**
**Wizara ya Maji**
**17 Septemba, 2021**

216468302

# TANGAZO

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## WIZARA YA MAJI

## TANGAZO LA NAFASI YA MWENYEKITI WA BODI YA MAJI YA BONDE LA ZIWA RUKWA

Katibu Mkuu, Wizara ya Maji anatangaza nafasi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Rukwa. Bodi hii inaundwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka 2009 chini ya Kifungu Na. 22. Muda wa Bodi ni miaka mitatu.

**MAJUKUMU YA BODI YA MAJI YA BONDE LA ZIWA RUKWA**

(a) Kuandaa mipango ya usimamizi wa rasilimali za maji, miradi, bajeti na mkakati wa utekelezaji wa Bonde;
(b) Kuunganisha mipango ya Wilaya kwenye mipango ya usimamizi wa rasilimali za maji ya Bonde;
(c) Kutoa miongozo na viwango vya ujenzi na matengenezo wa miundombinu ya vyanzo vya maji;
(d) Kufuatilia, kutathmini na kuidhinisha ujenzi na matengenezo wa miundombinu ya vyanzo vya maji;
(e) Kukusanya, kuchakata na kuchambua takwimu zinazohusu usimamizi wa rasilimali za maji;
(f) Kutunza na kuboresha tathmini za upatikanaji mahitaji ya rasilimali za maji;
(g) Kuidhinisha, kutoa na kufuta vibali vya kutumia maji na kutiririsha majitaka;
(h) Kutunza Daftari la Maji kulingana na Kifungu cha 78;
(i) Kufuatilia na kutekeleza vibali vya kutumia na kutiririsha majitaka na hatua za kuzuia uchafuzi;
(j) Kutatua migogoro ndani ya Bonde;
(k) Kutekeleza miradi na programu za usimamizi wa rasilimali za maji;
(l) Kuratibu shughuli za kisekta za usimamizi wa rasilimali za maji katika ngazi ya bonde na kuwa kiungo cha mawasiliano kati ya Sekta na watumiaji wa maji kwa ujumla;
(m) Kumshauri Mkurugenzi kwenye mambo ya kiufundi yanayohusu masuala ya maji shirikishi katika bonde;
(n) Kuteuwa Mwenyekiti na wajumbe wa kamati za dakio na kidakio maji; na
(o) Kutayarisha taarifa juu ya hali ya rasilimali za maji katika Bonde.

**SIFA ZA MWOMBAJI**

Mwombaji wa nafasi hii anatakiwa kuwa na ujuzi na uzoefu katika masuala ya Sekta ya Maji au Sekta zinazohusiana na sekta hiyo. Aidha, awe na ujuzi mahsusi kwenye masuala ya usimamizi wa rasilimali za maji na asiwe/ asitoke kwenye taasisi ambayo ni mtumiaji mkuu wa maji (Major Water User).

Maombi yatumwe kwa :

**Katibu Mkuu,**
**Wizara ya Maji,**
**Mji wa Serikali,**
**Mtaa wa Maji,**
**S.L.P. 456,**
**40473, DODOMA.**

Nakala ya maombi itumwe kupitia barua pepe: **ps@maji.go.tz**

Maombi yaambatishwe na wasifu wa mwombaji (CV) yenye wadhamini watatu na namba zao za simu. Andika **"Mwenyekiti Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Rukwa"** nyuma ya bahasha.

Mwisho wa kupokea maombi ni siku ya Ijumaa tarehe 15 Oktoba, 2021 saa 09.30 alasiri

**Imetolewana:**

**Katibu Mkuu**
**Wizara ya Maji**
**17 Septemba, 2021**

216468302

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## WIZARA YA MAJI

## TANGAZO LA NAFASI YA MWENYEKITI WA BODI YA MAJI YA BONDE LA ZIWA NYASA

Katibu Mkuu, Wizara ya Maji anatangaza nafasi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Nyasa. Bodi hii inaundwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka 2009 chini ya Kifungu Na. 22. Muda wa Bodi ni miaka mitatu.

**MAJUKUMU YA BODI YA MAJI YA BONDE LA ZIWA NYASA**

(a) Kuandaa mipango ya usimamizi wa rasilimali za maji, miradi, bajeti na mkakati wa utekelezaji wa Bonde;
(b) Kuunganisha mipango ya Wilaya kwenye mipango ya usimamizi wa rasilimali za maji ya Bonde;
(c) Kutoa miongozo na viwango vya ujenzi na matengenezo wa miundombinu ya vyanzo vya maji;
(d) Kufuatilia, kutathmini na kuidhinisha ujenzi na matengenezo wa miundombinu ya vyanzo vya maji;
(e) Kukusanya, kuchakata na kuchambua takwimu zinazohusu usimamizi wa rasilimali za maji;
(f) Kutunza na kuboresha tathmini za upatikanaji mahitaji ya rasilimali za maji;
(g) Kuidhinisha, kutoa na kufuta vibali vya kutumia maji na kutiririsha majitaka;
(h) Kutunza Daftari la Maji kulingana na Kifungu cha 78;
(i) Kufuatilia na kutekeleza vibali vya kutumia na kutiririsha majitaka na hatua za kuzuia uchafuzi;
(j) Kutatua migogoro ndani ya Bonde;
(k) Kutekeleza miradi na programu za usimamizi wa rasilimali za maji;
(l) Kuratibu shughuli za kisekta za usimamizi wa rasilimali za maji katika ngazi ya bonde na kuwa kiungo cha mawasiliano kati ya Sekta na watumiaji wa maji kwa ujumla;
(m) Kumshauri Mkurugenzi kwenye mambo ya kiufundi yanayohusu masuala ya maji shirikishi katika bonde;
(n) Kuteuwa Mwenyekiti na wajumbe wa kamati za dakio na kidakio maji; na
(o) Kutayarisha taarifa juu ya hali ya rasilimali za maji katika Bonde.

**SIFA ZA MWOMBAJI**

Mwombaji wa nafasi hii anatakiwa kuwa na ujuzi na uzoefu katika masuala ya Sekta ya Maji au Sekta zinazohusiana na sekta hiyo. Aidha, awe na ujuzi mahsusi kwenye masuala ya usimamizi wa rasilimali za maji na asiwe/ asitoke kwenye taasisi ambayo ni mtumiaji mkuu wa maji (Major Water User).

Maombi yatumwe kwa :

**Katibu Mkuu,**
**Wizara ya Maji,**
**Mji wa Serikali,**
**Mtaa wa Maji,**
**S.L.P. 456,**
**40473, DODOMA.**

Nakala ya maombi itumwe kupitia barua pepe: **ps@maji.go.tz**

Maombi yaambatishwe na wasifu wa mwombaji (CV) yenye wadhamini watatu na namba zao za simu. Andika **"Mwenyekiti Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Nyasa"** nyuma ya bahasha.
Mwisho wa kupokea maombi ni siku ya Ijumaa tarehe 15 Oktoba, 2021 saa 09.30 alasiri

**Imetolewana:**

**Katibu Mkuu**
**Wizara ya Maji**
**17 Septemba, 2021**

216468302

# TANGAZO

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## WIZARA YA MAJI

## TANGAZO LA NAFASI YA MWENYEKITI WA BODI YA MAJI YA BONDE LA WAMI/ RUVU

Katibu Mkuu, Wizara ya Maji anatangaza nafasi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Wami/ Ruvu. Bodi hii inaundwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka 2009 chini ya Kifungu Na. 22. Muda wa Bodi ni miaka mitatu.

**MAJUKUMU YA BODI YA MAJI YA BONDE LA WAMI/ RUVU**

(a) Kuandaa mipango ya usimamizi wa rasilimali za maji, miradi, bajeti na mkakati wa utekelezaji wa Bonde;
(b) Kuunganisha mipango ya Wilaya kwenye mipango ya usimamizi wa rasilimali za maji ya Bonde;
(c) Kutoa miongozo na viwango vya ujenzi na matengenezo wa miundombinu ya vyanzo vya maji;
(d) Kufuatilia, kutathmini na kuidhinisha ujenzi na matengenezo wa miundombinu ya vyanzo vya maji;
(e) Kukusanya, kuchakata na kuchambua takwimu zinazohusu usimamizi wa rasilimali za maji;
(f) Kutunza na kuboresha tathmini za upatikanaji mahitaji ya rasilimali za maji;
(g) Kuidhinisha, kutoa na kufuta vibali vya kutumia maji na kutiririsha majitaka;
(h) Kutunza Daftari la Maji kulingana na Kifungu cha 78;
(i) Kufuatilia na kutekeleza vibali vya kutumia na kutiririsha majitaka na hatua za kuzuia uchafuzi;
(j) Kutatua migogoro ndani ya Bonde;
(k) Kutekeleza miradi na programu za usimamizi wa rasilimali za maji;
(l) Kuratibu shughuli za kisekta za usimamizi wa rasilimali za maji katika ngazi ya bonde na kuwa kiungo cha mawasiliano kati ya Sekta na watumiaji wa maji kwa ujumla;
(m) Kumshauri Mkurugenzi kwenye mambo ya kiufundi yanayohusu masuala ya maji shirikishi katika bonde;
(n) Kuteuwa Mwenyekiti na wajumbe wa kamati za dakio na kidakio maji; na
(o) Kutayarisha taarifa juu ya hali ya rasilimali za maji katika Bonde.

**SIFA ZA MWOMBAJI**
Mwombaji wa nafasi hii anatakiwa kuwa na ujuzi na uzoefu katika masuala ya Sekta ya Maji au Sekta zinazohusiana na sekta hiyo. Aidha, awe na ujuzi mahsusi kwenye masuala ya usimamizi wa rasilimali za maji na asiwe/ asitoke kwenye taasisi ambayo ni mtumiaji mkuu wa maji (Major Water User).
Maombi yatumwe kwa :

**Katibu Mkuu,**
**Wizara ya Maji,**
**Mji wa Serikali,**
**Mtaa wa Maji,**
**S.L.P. 456,**
**40473, DODOMA.**

Nakala ya maombi itumwe kupitia barua pepe: **ps@maji.go.tz**

Maombi yaambatishwe na wasifu wa mwombaji (CV) yenye wadhamini watatu na namba zao za simu. Andika **"Mwenyekiti Bodi ya Maji Bonde la Wami/ Ruvu"** nyuma ya bahasha.

Mwisho wa kupokea maombi ni siku ya Ijumaa tarehe 15 Oktoba, 2021 saa 09.30 alasiri

**Imetolewana:**

**Katibu Mkuu**
**Wizara ya Maji**
**17 Septemba, 2021**

216468302

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## WIZARA YA MAJI

## TANGAZO LA NAFASI YA MWENYEKITI WA BODI YA MAJI YA BONDE LA PANGANI

Katibu Mkuu, Wizara ya Maji anatangaza nafasi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Pangani. Bodi hii inaundwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka 2009 chini ya Kifungu Na. 22. Muda wa Bodi ni miaka mitatu.

**MAJUKUMU YA BODI YA MAJI YA BONDE LA PANGANI**

(a) Kuandaa mipango ya usimamizi wa rasilimali za maji, miradi, bajeti na mkakati wa utekelezaji wa Bonde;
(b) Kuunganisha mipango ya Wilaya kwenye mipango ya usimamizi wa rasilimali za maji ya Bonde;
(c) Kutoa miongozo na viwango vya ujenzi na matengenezo wa miundombinu ya vyanzo vya maji;
(d) Kufuatilia, kutathmini na kuidhinisha ujenzi na matengenezo wa miundombinu ya vyanzo vya maji;
(e) Kukusanya, kuchakata na kuchambua takwimu zinazohusu usimamizi wa rasilimali za maji;
(f) Kutunza na kuboresha tathmini za upatikanaji mahitaji ya rasilimali za maji;
(g) Kuidhinisha, kutoa na kufuta vibali vya kutumia maji na kutiririsha majitaka;
(h) Kutunza Daftari la Maji kulingana na Kifungu cha 78;
(i) Kufuatilia na kutekeleza vibali vya kutumia na kutiririsha majitaka na hatua za kuzuia uchafuzi;
(j) Kutatua migogoro ndani ya Bonde;
(k) Kutekeleza miradi na programu za usimamizi wa rasilimali za maji;
(l) Kuratibu shughuli za kisekta za usimamizi wa rasilimali za maji katika ngazi ya bonde na kuwa kiungo cha mawasiliano kati ya Sekta na watumiaji wa maji kwa ujumla;
(m) Kumshauri Mkurugenzi kwenye mambo ya kiufundi yanayohusu masuala ya maji shirikishi katika bonde;
(n) Kuteuwa Mwenyekiti na wajumbe wa kamati za dakio na kidakio maji; na
(o) Kutayarisha taarifa juu ya hali ya rasilimali za maji katika Bonde.

**SIFA ZA MWOMBAJI**
Mwombaji wa nafasi hii anatakiwa kuwa na ujuzi na uzoefu katika masuala ya Sekta ya Maji au Sekta zinazohusiana na sekta hiyo. Aidha, awe na ujuzi mahsusi kwenye masuala ya usimamizi wa rasilimali za maji na asiwe/ asitoke kwenye taasisi ambayo ni mtumiaji mkuu wa maji (Major Water User).
Maombi yatumwe kwa :

**Katibu Mkuu,**
**Wizara ya Maji,**
**Mji wa Serikali,**
**Mtaa wa Maji,**
**S.L.P. 456,**
**40473, DODOMA.**

Nakala ya maombi itumwe kupitia barua pepe: **ps@maji.go.tz**

Maombi yaambatishwe na wasifu wa mwombaji (CV) yenye wadhamini watatu na namba zao za simu. Andika **"Mwenyekiti Bodi ya Maji Bonde la Pangani"** nyuma ya bahasha.

Mwisho wa kupokea maombi ni siku ya Ijumaa tarehe 15 Oktoba, 2021 saa 09.30 alasiri

**Imetolewana:**

**Katibu Mkuu**
**Wizara ya Maji**
**17 Septemba, 2021**

216468302

# TANGAZO

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## WIZARA YA MAJI

## TANGAZO LA NAFASI YA MWENYEKITI WA BODI YA MAJI YA BONDE LA KATI

Katibu Mkuu, Wizara ya Maji anatangaza nafasi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Kati. Bodi hii inaundwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka 2009 chini ya Kifungu Na. 22. Muda wa Bodi ni miaka mitatu.

**MAJUKUMU YA BODI YA MAJI YA BONDE LA KATI**

(a) Kuandaa mipango ya usimamizi wa rasilimali za maji, miradi, bajeti na mkakati wa utekelezaji wa Bonde;
(b) Kuunganisha mipango ya Wilaya kwenye mipango ya usimamizi wa rasilimali za maji ya Bonde;
(c) Kutoa miongozo na viwango vya ujenzi na matengenezo wa miundombinu ya vyanzo vya maji;
(d) Kufuatilia, kutathmini na kuidhinisha ujenzi na matengenezo wa miundombinu ya vyanzo vya maji;
(e) Kukusanya, kuchakata na kuchambua takwimu zinazohusu usimamizi wa rasilimali za maji;
(f) Kutunza na kuboresha tathmini za upatikanaji mahitaji ya rasilimali za maji;
(g) Kuidhinisha, kutoa na kufuta vibali vya kutumia maji na kutiririsha majitaka;
(h) Kutunza Daftari la Maji kulingana na Kifungu cha 78;
(i) Kufuatilia na kutekeleza vibali vya kutumia na kutiririsha majitaka na hatua za kuzuia uchafuzi;
(j) Kutatua migogoro ndani ya Bonde;
(k) Kutekeleza miradi na programu za usimamizi wa rasilimali za maji;
(l) Kuratibu shughuli za kisekta za usimamizi wa rasilimali za maji katika ngazi ya bonde na kuwa kiungo cha mawasiliano kati ya Sekta na watumiaji wa maji kwa ujumla;
(m) Kumshauri Mkurugenzi kwenye mambo ya kiufundi yanayohusu masuala ya maji shirikishi katika bonde;
(n) Kuteuwa Mwenyekiti na wajumbe wa kamati za dakio na kidakio maji; na
(o) Kutayarisha taarifa juu ya hali ya rasilimali za maji katika Bonde.

**SIFA ZA MWOMBAJI**

Mwombaji wa nafasi hii anatakiwa kuwa na ujuzi na uzoefu katika masuala ya Sekta ya Maji au Sekta zinazohusiana na sekta hiyo. Aidha, awe na ujuzi mahsusi kwenye masuala ya usimamizi wa rasilimali za maji na asiwe/ asitoke kwenye taasisi ambayo ni mtumiaji mkuu wa maji (Major Water User).

Maombi yatumwe kwa :

**Katibu Mkuu,**
**Wizara ya Maji,**
**Mji wa Serikali,**
**Mtaa wa Maji,**
**S.L.P. 456,**
**40473, DODOMA.**

Nakala ya maombi itumwe kupitia barua pepe: **ps@maji.go.tz**

Maombi yaambatishwe na wasifu wa mwombaji (CV) yenye wadhamini watatu na namba zao za simu. Andika **"Mwenyekiti Bodi ya Maji Bonde la Kati"** nyuma ya bahasha.

Mwisho wa kupokea maombi ni siku ya Ijumaa tarehe 15 Oktoba, 2021 saa 09.30 alasiri

**Imetolewana:**

**Katibu Mkuu**
**Wizara ya Maji**
**17 Septemba, 2021**

216468302

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## WIZARA YA MAJI

## TANGAZO LA NAFASI YA MWENYEKITI WA BODI YA MAJI YA BONDE LA RUVUMA NA PWANI YA KUSINI

Katibu Mkuu, Wizara ya Maji anatangaza nafasi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Ruvuma na Pwani ya Kusini. Bodi hii inaundwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka 2009 chini ya Kifungu Na. 22. Muda wa Bodi ni miaka mitatu.

**MAJUKUMU YA BODI YA MAJI YA BONDE LA RUVUMA NA PWANI YA KUSINI**

(a) Kuandaa mipango ya usimamizi wa rasilimali za maji, miradi, bajeti na mkakati wa utekelezaji wa Bonde;
(b) Kuunganisha mipango ya Wilaya kwenye mipango ya usimamizi wa rasilimali za maji ya Bonde;
(c) Kutoa miongozo na viwango vya ujenzi na matengenezo wa miundombinu ya vyanzo vya maji;
(d) Kufuatilia, kutathmini na kuidhinisha ujenzi na matengenezo wa miundombinu ya vyanzo vya maji;
(e) Kukusanya, kuchakata na kuchambua takwimu zinazohusu usimamizi wa rasilimali za maji;
(f) Kutunza na kuboresha tathmini za upatikanaji mahitaji ya rasilimali za maji;
(g) Kuidhinisha, kutoa na kufuta vibali vya kutumia maji na kutiririsha majitaka;
(h) Kutunza Daftari la Maji kulingana na Kifungu cha 78;
(i) Kufuatilia na kutekeleza vibali vya kutumia na kutiririsha majitaka na hatua za kuzuia uchafuzi;
(j) Kutatua migogoro ndani ya Bonde;
(k) Kutekeleza miradi na programu za usimamizi wa rasilimali za maji;
(l) Kuratibu shughuli za kisekta za usimamizi wa rasilimali za maji katika ngazi ya bonde na kuwa kiungo cha mawasiliano kati ya Sekta na watumiaji wa maji kwa ujumla;
(m) Kumshauri Mkurugenzi kwenye mambo ya kiufundi yanayohusu masuala ya maji shirikishi katika bonde;
(n) Kuteuwa Mwenyekiti na wajumbe wa kamati za dakio na kidakio maji; na
(o) Kutayarisha taarifa juu ya hali ya rasilimali za maji katika Bonde.

**SIFA ZA MWOMBAJI**

Mwombaji wa nafasi hii anatakiwa kuwa na ujuzi na uzoefu katika masuala ya Sekta ya Maji au Sekta zinazohusiana na sekta hiyo. Aidha, awe na ujuzi mahsusi kwenye masuala ya usimamizi wa rasilimali za maji na asiwe/ asitoke kwenye taasisi ambayo ni mtumiaji mkuu wa maji (Major Water User).

Maombi yatumwe kwa :

**Katibu Mkuu,**
**Wizara ya Maji,**
**Mji wa Serikali,**
**Mtaa wa Maji,**
**S.L.P. 456,**
**40473, DODOMA.**

Nakala ya maombi itumwe kupitia barua pepe: **ps@maji.go.tz**

Maombi yaambatishwe na wasifu wa mwombaji (CV) yenye wadhamini watatu na namba zao za simu. Andika **"Mwenyekiti Bodi ya Maji Bonde la Ruvuma na Pwani ya Kusini"** nyuma ya bahasha.

Mwisho wa kupokea maombi ni siku ya Ijumaa tarehe 15 Oktoba, 2021 saa 09.30 alasiri

**Imetolewana:**

**Katibu Mkuu**
**Wizara ya Maji**
**17 Septemba, 2021**

216468302



# BAKWATA yaomba mashehe, maimamu kuhamasisha sensa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MWENYEKITI wa Halmashauri Kuu ya Baraza la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Wilaya ya Dodoma, Bashiru Omary, amewaomba mashehe, maimamu na walimu wa madrasaa kuisaidia serikali kuhamasisha waumini wao kushiriki Sensa ya Watu na Makazi Agosti, 2022.

Bashiru alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari, kuhusu wito uliotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan, baada ya kuzindua mwongozo wa uelimishaji na uhamasishaji wa sensa hiyo.

Alisema kuwa viongozi hao wana jukumu kubwa la kuhakikisha zoezi hilo linafanikiwa ili serikali iweze kupanga majukumu yake ya kimaendeleo kwa wananchi wake.

Aidha, alisema serikali inapaswa kufahamu idadi ya wananchi wake ili kupanga mipango ambayo itakayowaletea maendeleo, hivyo ni wajibu mkubwa kuhakikisha viongozi hao wa dini wanatoa ushirikiano kikamilifu.

Mwenyekiti huyo wa BAKWATA wilaya, pia alisema nchi yoyote bila kufanya sensa ya watu na makazi yake kamwe haiwezi kufikia maendeleo kwa wananchi wake.

"Hivyo niwaombe viongozi ngazi ya mashehe, maimamu na walimu wa madrasa kwenye vituo vyao vya kazi wajiandae na sensa hiyo wakati itakapowadia kuhakikisha watu wote wanahesabiwa ikiwa na pamoja watu wao kutoa ushirikiano kwa maofisa walioteuliwa kuifanya kazi hiyo kwa niaba ya serikali," alisema.

Pia, alisema kutokana na hali hiyo, viongozi hao wanapaswa kutambua kuwa suala la sensa lipo kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wake, hivyo wakumbuke kuwa ushiriki wao wa kuhamasisha watu unategemewa sana na serikali.

Hata hivyo, aliwataka mashehe, maimamu na walimu wa madrasa kutohusisha suala hilo la sensa ya watu na makazi na itikadi yoyote ya kidini, siasa wala kabila, kwani zoezi hili lipo kwa ajili ya maendeleo ya watu wote.

# Utambuzi wa watoto wenye mahitaji maalum watakiwa

**Na Mwandishi Wetu,** CHAMWINO

SERIKALI kwa kushirikiana na wananchi imetakiwa kutumia njia mbadala kutambua idadi ya watoto wenye mahitaji maalum ili kuwaandikishwa shule za watoto wenye mahitaji maalumu.

Kwa mujibu wa ripoti iliyotolewa na wakazi wa wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma baada ya uchambuzi uliofanywa na Shirikia lisilo la Kiserikali la ACTION AID Tanzania, ili kufanikisha malengo ya kila mtoto aliyefikisha miaka ya kuandikishwa shule, serikali ina wajibu kuhakikisha shule zilizotengwa ziwe na miundombinu wezeshi.

Akisoma taarifa ya uchambuzi huo, Ester Maile, alisema serikali itoe ruzuku kwa kila shule kulingana na idadi ya wanafunzi na pia watoto wenye ulemavu waongezewe kiasi cha ruzuku ili kukidhi mahitaji yao.

Pia, alisema serikali itoe au kupunguza kodi kwenye vifaa vinavyotumiwa na wanafunzi wenye mahitaji maalum mfano bei ya viti mwendo huuzwa kwa Sh. 250,000 hicho ni kiasi kikubwa familia nyingi zinashindwa kununua.

Maile alisema katika kuchambuzi huo idadi ya watoto wenye mahitaji maalumu walioandikishwa shule ni 81, ambao hawajaandikishwa 80, hali hiyo ni hatari kwa taifa lijalo kwani kutakuwa na ongezeko kubwa la watoto ambao watakuwa tegemezi.

Maile alisema katika Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino kati ya shule 20 zilizotembelewa zinauhitaji wa madarasa 374, sawa na asilimia 49.73 ya uhaba unapelekea kusomea chini ya miti mfano Shule ya Msingi Mapinduzi.

"Serikali pamoja na wadau wa elimu kujenga miundombinu ambayo ni rafiki kwa wanafunzi wote mfano baadhi ya madarasa hayana ngazi mserereko kwa ajili ya watoto wanaotumia viti mwendo," alisema Maile.

Alisema umbali wa shule kufikiwa kwa wanafunzi wote bado ni changamoto kwani baadhi zipo umbali mrefu kutoka kwenye makazi ya watu, hivyo husababisha watoto kukosa vipindi msimu wa mvua.

"Mfano Shule ya Mloda kwa watoto wanaotoka kitongoji cha Maumi wanafunzi hutembea umbali mrefu takribani kilomenta 15 umbali wa kwenda na kurudi," alisema.

Aliongeza kuwa Halmashauri ya Wilaya hiyo kuna uhaba mkubwa wa matundu ya vyoo ukilinganisha na namba ya matundu yaliyopo.

Alisema uhitaji wa matundu ya vyoo kwa shule 20 zilizotembelewa ni matundu 653 wakati yaliyopo ni matundu 205 ikiwa upungufu ni 448.

"Kwa shule 20, zilizofanyiwa uchambuzi katika zoezi hili imefahamika kuwa kuna uhitaji wa madawati 6,470, lakini yaliyopo ni 3,328 huku upungufu ni madawati 3,142 sawa na asilimia 48.56," alisema.

Diwani wa Kata ya Chilonwa, Alfa Mtura na Diwani wa Kata ya Iringa Mvumi walikiri kuwapo kwa changamoto hizo katika elimu.

Ofisa Mipango wa Halmashauri hiyo, John Masero, alisema pamoja na serikali kuhimiza wananchi kujenga maboma ili itoe fedha kwa ajili ya kuyakamilisha, katika wilaya hiyo imekuwa ni changamoto kutokana na umaskini wa watu wake.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAJI**

**TANGAZO LA NAFASI YA MWENYEKITI WA BODI YA MAJI YA BONDE LA RUFIJI**

Katibu Mkuu, Wizara ya Maji anatangaza nafasi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Rufiji. Bodi hii inaundwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka 2009 chini ya Kifungu Na. 22. Muda wa Bodi ni miaka mitatu.

**MAJUKUMU YA BODI YA MAJI YA BONDE LA RUFIJI**

(a) Kuandaa mipango ya usimamizi wa rasilimali za maji, miradi, bajeti na mkakati wa utekelezaji wa Bonde;
(b) Kuunganisha mipango ya Wilaya kwenye mipango ya usimamizi wa rasilimali za maji ya Bonde;
(c) Kutoa miongozo na viwango vya ujenzi na matengenezo wa miundombinu ya vyanzo vya maji;
(d) Kufuatilia, kutathmini na kuidhinisha ujenzi na matengenezo wa miundombinu ya vyanzo vya maji;
(e) Kukusanya, kuchakata na kuchambua takwimu zinazohusu usimamizi wa rasilimali za maji;
(f) Kutunza na kuboresha tathmini za upatikanaji mahitaji ya rasilimali za maji;
(g) Kuidhinisha, kutoa na kufuta vibali vya kutumia maji na kutiririsha majitaka;
(h) Kutunza Daftari la Maji kulingana na Kifungu cha 78;
(i) Kufuatilia na kutekeleza vibali vya kutumia na kutiririsha majitaka na hatua za kuzuia uchafuzi;
(j) Kutatua migogoro ndani ya Bonde;
(k) Kutekeleza miradi na programu za usimamizi wa rasilimali za maji;
(l) Kuratibu shughuli za kisekta za usimamizi wa rasilimali za maji katika ngazi ya bonde na kuwa kiungo cha mawasiliano kati ya Sekta na watumiaji wa maji kwa ujumla;
(m) Kumshauri Mkurugenzi kwenye mambo ya kiufundi yanayohusu masuala ya maji shirikishi katika bonde;
(n) Kuteuwa Mwenyekiti na wajumbe wa kamati za dakio na kidakio maji; na
(o) Kutayarisha taarifa juu ya hali ya rasilimali za maji katika Bonde.

**SIFA ZA MWOMBAJI**

Mwombaji wa nafasi hii anatakiwa kuwa na ujuzi na uzoefu katika masuala ya Sekta ya Maji au Sekta zinazohusiana na sekta hiyo. Aidha, awe na ujuzi mahsusi kwenye masuala ya usimamizi wa rasilimali za maji na asiwe/ asitoke kwenye taasisi ambayo ni mtumiaji mkuu wa maji (Major Water User).

Maombi yatumwe kwa :

**Katibu Mkuu,**
**Wizara ya Maji,**
**Mji wa Serikali,**
**Mtaa wa Maji,**
**S.L.P. 456,**
**40473, DODOMA.**

Nakala ya maombi itumwe kupitia barua pepe: **ps@maji.go.tz**

Maombi yaambatishwe na wasifu wa mwombaji (CV) yenye wadhamini watatu na namba zao za simu. Andika **"Mwenyekiti Bodi ya Maji Bonde Rufiji"** nyuma ya bahasha.

Mwisho wa kupokea maombi ni siku ya Ijumaa tarehe 15 Oktoba, 2021 saa 09.30 alasiri

**Imetolewana:**

**Katibu Mkuu**
**Wizara ya Maji**
**17 Septemba, 2021**

216468302





# ‘Watoto walindwe kuwaepusha na maambukizi Virusi Ukimwi’

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Ukimwi, Kifua Kikuu, Dawa za Kulevya na magonjwa yasiyoambukiza imewataka wazazi na walezi nchini kuwalea watoto katika mazingira yatakayowaepusha kujiingiza kwenye vitendo vya kupata maambukizi ya virusi vya Ukimwi.

Aidha, imewataka kuwaepusha watoto wao kujiingiza kwenye matumizi ya dawa za kulevya kwa kuwa vinaharibu nguvukazi ya taifa na kuliingiza taifa hasara kutokana na kuwahudumia waathirika wa dawa hizo.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Fatma Hassan Tawfiq, aliyasema hayo juzi jijini hapa wakati wa chakula cha pamoja kati ya wajumbe wa kamati hiyo, wazazi na watumishi wa Shule ya Paradise Mission Pre and Primary School, iliyopo katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi kilichoandaliwa na shule hiyo.

Alisema kwa sasa kundi la wasichana wenye umri wa kuanzia miaka 15 mpaka 24 ndilo lipo kwenye hatari zaidi ya kupata maambukizi ya virusi vya Ukimwi na kwamba kuna kila sababu kundi hilo kulindwa ikiwa ni pamoja na kupewa elimu ya namna ya kujilinda.

“Mbeya ni miongoni mwa mikoa ambayo takwimu za maambukizi ya Ukimwi ziko juu sana, hivyo tumekuja kufuatilia afua mbalimbali, lakini tumeona ni vyema tuungane nanyi wazazi wenzetu kwenye hii hafla ili tupeane mawili matatu kuhusu haya mambo,” alisema Tawfiq.

Aliwataka Watanzania kujitokeza kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ili kupima afya zao na kwamba kwa wale wanaobainika kuwa wana maambukizi ya Ukimwi waingizwe kwenye matumizi ya dawa za kufubaza virusi hivyo.

Aliupongeza uongozi wa Shule ya Paradise Mission Pre and Primary School kwa kuwakutanisha wazazi na walezi kwa ajili ya kupeana elimu akidai kuwa utaratibu huo unasaidia kuboresha malezi ya watoto huku akiwataka walimu pia kuendelea kuwasaidia watoto.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa shule hiyo, Ndele Mwaselela, aliishukuru kamati ya Bunge kwa kujitolea kutoa elimu kwa wazazi ambayo alisema kwa sasa malezi ya watoto ni muhimu kutokana na mabadiliko ya teknolojia.

Alisema ili kuhakikisha watoto wanaosoma kwenye shule hiyo wanapata malezi bora, wameajiriwa watumishi maalumu kwa ajili ya kuwalea na kuhakikisha kipindi cha likizo wanawarejesha nyumbani wakiwa salama.

Alisema ushirikiano wa wazazi, walezi na uongozi wa shule kwenye malezi ya watoto ni jambo muhimu na ndiyo sababu iliyoufanya uongozi wa shule hiyo kuandaa hafla hiyo ya chakula cha jioni.

“Sasa hivi tuna usafiri wa mabasi yetu ya kuwarejesha watoto nyumbani wakati wa likizo, tumeacha ule utaratibu wa kutumia mabasi ya abiria wengine kusafirisha watoto kwa sababu tumebaini inakuwa usumbufu kwa wazazi na tumeajiri watumishi wa kusafiri pamoja na hawa watoto,” alisema Mwaselela.

Aliiomba Kamati hiyo ya Bunge kuendelea kutoa elimu kwa wazazi ili kuhakikisha malezi ya watoto yanakuwa bora na yanakuwa ni yale ya kuwasaidia watoto kuepuka vitendo ambavyo vitawaathiri kimwili na kisaikolojia.



Baadhi ya wazazi na walezi wa watoto wanaosoma Shule ya awali na Msingi ya Paradise Mission iliyoko Mbalizi mjini Mbeya wakimsikiliza Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ukimwi, Kifua Kikuu, Dawa za Kulevya na magonjwa yasiyoambukizwa, Fatuma Tawfiq, katika chakula cha jioni kilichoandaliwa na shule hiyo juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mil. 200/- zatolewa kukamilisha mradi wa maji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa Kijiji cha Ilota, Kata ya Mshewe Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wanatarajiwa kuondokana na tatizo la muda mrefu la uhaba wa maji baada ya utekelezaji wa mradi wa kupeleka maji kwenye kijiji hicho kutoka Mbalizi kuanza kutekelezwa.

Serikali imetoa Sh. milioni 200 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo ambao ni wa kupeleka maji kwa njia ya mseleleko kutoka katika mradi wa Shongo unaohudumia Mbalizi na Bonde la Songwe.

Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, Oran Njeza, aliyasema hayo juzi alipofanya ziara ya kukagua utekelezaji wa mradi huo pamoja na kuzungumza na wananchi wa kijiji hicho kwa ajili ya kuwapa matumaini.

Alisema mtaro wa kupeleka maji katika kijiji hicho unachimbwa na vijana kutoka Mbalizi na kwamba endapo itaonekana wanachelewa kumaliza watachukuliwa vijana kutoka katika maeneo mengine ili waungane na wa kijiji hicho.

“Kinachochelewesha vijana wetu kuchelewa kufika ni kwa sababu ardhi kwa kipindi hiki ni ngumu, lakini wakikazana tunaweza kupata maji ndani ya wiki tatu hivyo nawaomba tuongeze ushirikiano kwenye hili jambo,” alisema Njeza.

Baadhi ya wanawake wa kijiji hicho walisema hawajawahi kupata maji ya bomba na badala yake wamekuwa wakihangaika kwenda kuchota makorongoni ambako hawana uhakika na usalama wake.

Mmoja wa wananchi hao, Juma Ndamile, aliiomba serikali kuwaajiri vijana wa maeneo mengine ili kuharakisha kuchimba mtaro huo na wananchi waanze kupata maji haraka.

Alisema maji kwenye kijiji hicho ni tatizo la muda mrefu hasa kipindi cha kiangazi ambacho amedai yanakauka na kuwalazimu wanawake kutumia muda mrefu kwenda kuchota yaliyotuwama kwenye makorongo.

Alisema wakati mwingine wamekuwa wakiumwa matumbo bila kujua sababu na kwamba kuna uwezekano chanzo ikawa ni aina ya maji wanakunywa.

“Tunajua kwamba hii ni ajira kwa vijana wetu, lakini lengo letu tupate maji haraka, kama inawezekana tunaiomba serikali itusaidie hata vijana wa maeneo mengine ili kazi iishe haraka tuanze kunywa maji ya bomba,” alisema Njeza.

# TUGHE yaomba serikali taarifa madai ya walimu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imeombwa kutoa taarifa za mara kwa mara kuhusu namna inavyoshughulikia madai ya wafanyakazi hasa walimu ili kuongeza ari na ufanisi wa kazi kwa watumishi hao pamoja na kupunguza migogoro kazini.

Ombi hilo lilitolewa jijini hapa mwishoni mwa wiki na Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa serikalini na Afya Tanzania (TUGHE), Hery Mkunda, wakati wa Mkutano Mkuu wa Baraza la Vyama vya TUGHE na Chama cha walimu (CWT).

Alisema tatizo kubwa lipo kwenye Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwamba kitendo cha kutotoa taarifa haraka huwa kinasababisha manung’uniko miongoni mwa watumishi wenye madai na hivyo kupunguza hata ufanisi wa kazi.

Mkunda alisema wakati mwingine watumishi huwa wanawasilisha malalamiko yao mapema, lakini yasiposhughulikiwa kwa wakati na hata taarifa za namna yanavyoshughulikiwa huwa wanaanza kuwa na wasiwasi na kutumia muda mwingi kuhangaikia malalamiko hayo badala ya kufanya kazi.

“Mtumishi huwa anatamani kujua namna madai yake yanavyoshughulikia, tunaomba wizara iwe inatoa taarifa ili mhusika ajuwe kwamba madai yake yamefikia hatua gani, ikiwa hivyo mtakuwa mmetusaidia sana,” alisema Mkunda.

Nao baadhi ya wajumbe wa baraza hilo walisema endapo serikali itakuwa inatoa taarifa hizo mapema, itaongeza tija kwenye uwajibikaji wa watumishi hao na kuondoa malalamiko ya mara kwa mara ambayo wakati mwingine yanapunguza ufanisi.

Mmoja wa wajumbe hao, Benedict Raymond, alisema lengo la baraza hilo ni kuhakikisha migogoro inaisha na wafanyakazi wote wanafanya kazi wakiwa na moyo mmoja na wafanye kazi ambazo zitawafanya watimize malengo ya serikali.

Alisema endapo serikali inakuwa na malengo yake yanayotakiwa kutekelezwa na wafanyakazi wenye manung’uniko, kuna hatari ya matokeo yanayokusudiwa yasifikiwe.

Akijibu malalamiko ya wajumbe wa Baraza hilo, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. James Mdoe, aliwataka wafanyakazi wawe na subira wakati serikali ikiendelea kushughulikia madai yao.

Prof. Mdoe alikiri uwapo wa malalamiko mbalimbali ya watumishi huku akidai kuwa yanaendelea kushughulikiwa kwenye hatua mbalimbali na taarifa zitaendelea kutolewa kulingana na namna madai hayo yanavyoshughulikiwa.

Aliwataka wafanyakazi hao kuendelea kutoa huduma kwa Watanzania kwa mujibu wa maelekezo na miongozo ya kazi zao wakati wakisubiri mrejesho wa namna madai yao yanavyoshughulikiwa.

“Tunawaomba sana wakati huu ambao madai yenu yanashughulikiwa mtupe ushirikiano wa kutosha ili kusiwe na vikwazo vya aina yoyote wakati wa kushughulikia madai haya na tuhimizane kazi ziendelee kufanyika za kuwahudumia Watanzania,” alisema Prof. Mdoe.



# Wakulima washauriwa mazao ya viungo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo, Maliasili na Mifugo imewataka wakulima kujikita zaidi katika kilimo cha viungo ambacho soko lake la nje ni la uhakika ikiwamo vanila.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Wizara hiyo, Dk. Soud Nahoda, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Mahonda, Asha Abdalla Mussa, aliyetaka kujua wizara imejipanga vipi kuwawezesha wakulima kulima kilimo cha mazao ya viungo chenye tija.

Dk. Nahoda alisema Zanzibar imejipanga kurudisha hadhi yake ya miaka ya nyuma kuwa kisiwa kinachoongoza kwa uzalishaji na usafirishaji wa mazao ya viungo.

Aliyataja mazao ya viungo ambayo Zanzibar ilipata umaarufu mkubwa kiasi ya kuitwa kisiwa cha viungo ni pilipili manga, mbata inayozalisha mafuta ya nazi pamoja na karafuu.

Aliyataja mazao mengine ya viungo yaliyoipatia sifa kubwa Zanzibar katika miaka ya 1960 ni hiliki, manjano na mdalasini ambavyo soko lake kubwa lilikuwa katika nchi za Bara la Hindi.

Alisema kazi kubwa inayofanywa kwa sasa ni wizara kwa kushirikiana na Umoja wa Ulaya (EU) kutekeleza mradi wa viungo ambao utawawezesha wakulima kulima mazao hayo.

"Tumeanza kazi ya kuhamasisha wakulima wetu Unguja na Pemba kujikita katika kilimo cha mazao ya viungo ambapo upo mradi unatekelezwa na EU wa kuwapatia mbegu wakulima," alisema.

"Mheshimiwa Spika, tumeanza kuwahamasisha wakulima wetu kulima kilimo cha mazao ya viungo chenye tija kubwa kupitia mradi wa viungo unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya," alisema waziri huyo.

Aidha, alieleza kuwa mradi huo wa mazao ya viungo ambayo yamepewa kipaumbele na wakulima kutakiwa kujikita zaidi na zao la vanila ambapo bei yake ipo juu na soko lake ni la uhakika.

Alisema katika mradi wa mazao ya viungo unaotekelezwa na EU wakulima wamepatiwa mbegu za vanila huku wakipatiwa mbinu za kisasa kulima zao hilo.

Utafiti uliofanywa umeonyesha kwamba mazao ya viungo yamekuwa na soko kubwa nchini na katika nchi mbalimbali za Ulaya kufuatia kuimarika kwa sekta ya utalii.

## Uvuvi haramu tishio uchumi wa bluu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Uvuvi na Uchumi wa Bluu, Abdalla Hussein Kombo, amesema uvuvi haramu ni miongoni mwa tishio la athari kubwa za mazingira na maendeleo ya uchumi wa bluu.

Kombo alisema hayo jana wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Kojani, Hassan Omar Hamadi, aliyetaka kujua wizara kwa kiasi gani imejipanga kupambana na uvuvi haramu kuelekea uchumi wa bluu.

Kombo alisema uvuvi haramu haukubaliki moja kwa moja katika mikakati ya kuelekea uchumi wa bluu kwa sababu unaathiri maliasili na rasilimali za baharini.

Alisema baadhi ya wavuvi bado wanajishughulisha na uvuvi haramu wa kuvua samaki kwa kutumia nyavu zenye macho madogo ambazo hunasa samaki wa aina mbalimbali ikiwamo wadogo ambao hawafai kwa matumizi ya kula.

Aidha, alisema uvuvi wa kutumia mishale na vioo vya kuzamia chini ya bahari haukubaliki kwa sababu ni tishio kwa athari na uharibifu wa matumbawe.

"Uvuvi wa kuzamia chini ya bahari ni maarufu kwa wavuvi wengi wa mwambao wa pwani ambao, athari zake kubwa ni kuvunja matumbawe na matokeo yake kusababisha uhaba wa samaki kukimbia," amesema.

Aliwataja baadhi ya samaki ambao wamepungua kwa kiasi kikubwa kutokana na athari za uharibifu wa matumbawe ni pweza, ngisi pamoja na kamba.

"Samaki hawa ni maarufu wenye soko kubwa la kitalii, lakini wapo katika tishio kubwa la kutoweka kutokana na uharibifu wa matumbawe ambayo ni nyumba za samaki hao," alisema.

Waziri huyo alisema, wameanza kutoa mafunzo kwa wavuvi wa aina mbalimbali kutunza mazingira ya baharini, huku wavuvi wakiheshimu na kuacha kuvua samaki katika maeneo ambayo yametengwa kwa hifadhi ya uvuvi.

Alisema katika kisiwa cha Zanzibar tayari eneo lote la baharini lipo chini ya hifadhi ya uvuvi ambapo wavuvi wanapaswa kuheshimu sheria za uvuvi zinazosisitiza kulinda mazingira.



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Makazi, Riziki Pembe Juma, akizungumza na Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Dk. Khalid Salum Muhammed, nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi Chukwani Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Ardhi aliyogawa Abeid Karume sasa kuhakikiwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Riziki Pembe Juma, amesema Serikali ya Zanzibar imeanza kuhakiki eka tatu zilizotolewa na mwasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar, Hayati Abeid Amani Karume.

Kati ya hizo, baadhi yake wananchi wamebadilisha matumizi yake na kuwa ya makazi ya kudumu.

Waziri Pembe aliyasema hayo wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini, Machano Othman Said, aliyetaka kujua matumizi ya eka tatu yakoje baada ya kujitokeza tabia ya kuvamia maeneo hayo.

Pembe alikiri kuwapo kwa uvamizi wa ardhi ya eka tatu zilizotolewa baada ya Mapinduzi ya Januari 12, mwaka 1964 ambapo ardhi ilitaifishwa na kugawiwa kwa wananchi wazalendo.

Alisema umejitokeza uvamizi mkubwa wa ardhi wa ekari tatu ambazo wananchi wamebadilisha matumizi yake kutoka kilimo hadi kuwa makazi ya kudumu ya wananchi.

Aliyataja maeneo ambayo wananchi wamebadilisha hati za matumizi ya eka tatu ni Kinyasini, Mwakaje, Mbuzini, Mfenesini pamoja na Mwera Tunguu kutokana na kasi ya mahitaji ya makazi ya wananchi.

Pembe alisema zoezi la uhakiki limeanza ambapo watu waliopewa ekari tatu wote wanatakiwa kujisajili kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa ikiwamo kwenda katika ofisi ya wilaya ya eneo ambalo ardhi hiyo imetolewa.

Aidha, alisema ni marufuku mtu yeyote kuuza ekari tatu au kukodisha kwa matumizi mengine na ekari tatu kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ipo chini ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MATANGAZO MCHANGANYIKO**

PATA MKOPO WA HARAKA KWA
MASHARTI NAFUU KUTOKA ENTEPRISES
FINANCE LIMITED (EFL).
KWA MAWASILIANO ZAIDI
**TUPIGIE:0677 111 333**
**AU 0758 112 332**

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676



**SHUKRAN**

Familia ya Marehemu Shabani Shimbo Mgonja wa Corridor Area, Arusha inawashukuru ndugu jamaa, marafiki, vikundi vyote na watu wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine katika kumpumzisha Mama yetu mpendwa

**AMINA SHABANI MGONJA**

Aliyeitwa na Mungu tarehe 10 August 2021 na kuzikwa tarehe 13 August 2021 huko Gonja Maore, Same. Si rahisi kuwataja wote, tunawaomba hawa wachache wawakilishe, Dr. Julius na wauguzi wa Moyo Medical Care; madaktari na wauguzi wa hospitali ya Selian, Arusha; Umoja wa Wapare wa Maore, Arusha; Umoja wa kinamama Estate ya Kijenge, Arusha; JKT-Arusha; Jumuiya ya Waislamu Kijenge na Gonja Maore; Wanakijiji wa Gonja Maore; Familia ya Makange, DSM; Mzee Khalifa Mgonja, Arusha; Wafanyakazi wa TANESCO (Mameneja wa mikoa, idara ya mafunzo na umoja wa Wanawake Wahandisi); Arusha RV friends; Obay Primary Mates na kikundi cha Tupendane Pretty family, Arusha. Familia inachukua nafasi hii kuwajulisha kuwa jumamosi asubuhi tarehe 25 September 2021, kutakuwa na DUA kwenye nyumba ya familia huko Gonja Maore,Same. Wote mnakaribishwa kwenye DUA.

***"Inna Lillah Wa inna Illaihi Rajioun"***

116469802



**SHUKRAN**

Familia ya Marehemu Shabani Shimbo Mgonja wa Corridor Area, Arusha inawashukuru ndugu jamaa, marafiki, vikundi vyote na watu wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine katika kumpumzisha mdogo wao mpendwa

**HAJI SHABANI MGONJA**

Aliyeitwa na Mungu tarehe 18 August 2021 na kuzikwa tarehe 21 August 2021 huko Gonja Maore, Same. Si rahisi kuwataja wote, tunawaomba hawa wachache wawakilishe, Umoja wa Wapare wa Maore, Arusha; Umoja wa kina mama Estate ya Kijenge, Arusha; JKT-Arusha;Jumuiya ya Waislamu Kijenge na Gonja Maore; Wanakijiji wa Gonja Maore; Familia ya Makange, DSM; Mzee Khalifa Mgonja, Arusha; Arusha RV friends na kikundi cha Tupendane Pretty family, Arusha. Familia inachukua nafasi hii kuwajulisha kuwa jumamosi asubuhi tarehe 25 September 2021, kutakuwa na DUA kwenye nyumba ya familia huko Gonja Maore Same. Wote mnakaribishwa kwenye DUA.

***"Inna Lillah Wa inna Illaihi Rajioun"***

116469802

## KUPOTEA KWA CHETI



**CAROLINE EMANUEL MUYA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.2375/0016** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **KANDOTO GIRLS SCIENCE SEKONDARI mwaka 2013.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.Taarifa ya polisi: **DAR/MAG/RB/455799/2021.**

116469602

**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MWANZA**
**WILAYA YA NYAMAGANA MWANZA**
**SHAURI LA MIRATHI NO 16/2021**

**MWOMBAJI…………………1. NATHAN MUNAI OMUTITI**
**2. SENORINA ALOYCE MBOYA**

**MAREHEMU……………… GODFREY MAKUTWA OMUTITI**

**KWA: YEYOTE ANAEHUSIKA**

**KUITWA SHAURINI**

Mwombaji tajwa hapo juu amefungua shuri la mirathi ya marehemu **GODFREY MAKUTWA OMUTITI** katika mahakama hii hati za mirathi zinapatikana katika mahakama hii.

Tunaomba yeyote mwenyepingamizi katika mirathi hii anatakiwa kuhudhuria mahakamani tarehe 01/10/2021 saa 2:00 asubuhi ninyi/ wewe binafsi au wakili wenu kisheria.

**Zingatia** kwamba kutohudhuria kwenu kwa tarehe tajwa kesi hii itaendelea bila ninyi kuwepo mahakamani.

Imetolewa kwa mkono wangu na muhuri wa mahakama hii leo tarehe 06/09/2021.

**HAKIMU MKAZI**
**WILAYA YA NYAMAGANA.**
**MWANZA**

116464602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA BUKOBA - KAGERA**

**MAOMBI MADOGO NA. 225/2021**

**VERONICA METHOD ……………..MWENYE TUZO**

**DHIDI YA**

**AMOSI MUKYANUZI …………MSHINDWA HUKUMU**

**KWA: AMOSI MUKYANUZI (POPOTE PALE ULIPO)**

Unaarifiwa kuwa kesi Na. 225/2021 imepangwa kutajwa tarehe 09/11/2021 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza R. Mtei saa 2:00 asubuhi, mahali - Bukoba Mjini. Hivyo, unaamuriwa kuhudhuria wewe mwenyewe/mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja na hukumu kutolewa dhidi yako.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 02/09/2021.

**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA BUKOBA**

116468902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya Mwanzo PONGWE**

**Usimamizi wa Mirathi No. 34/2021**

**Ombi la GEOFREY JOHN MGAYA Kuteuliwa**

**Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu**
**LUNYAMACHO WILLIAM MGAYA**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 6/10/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 16/09/2021.

Sahihi ya Hakimu

116469702

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

116460202

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Rais Hichilema asifiwa kwa msafara mdogo

**New York,** MAREKANI

RAIS wa Zambia, Hakainde Hichilema (pichani chini), amesifiwa mitandaoni kwa kusafiri na maofisa wachache, ili kuhudhuria kikao cha 76 za mkutano wa Baraza la Kuu la Umoja wa Mataifa, jijini New York.

Hichilema alisafiri kwa kutumia ndege ya Qatar Airways kutoka mjini Lusaka, akiandamana na mawaziri wawili.

"Kama nilivyoahidi kabla niingie madarakani, nitahakikisha usimamizi mzuri wa rasilimali za umma na kwa hivyo tumesafiri na timu konda ambayo inaundwa na mawaziri wa Mambo ya Nje na Fedha, Stanley Kakubo na Dk. Situmbeko Musokotwane mtawaliwa," alisema katika taarifa kabla ya kuondoka. **BBC**



Maelfu ya wahamiaji wakisubiri hatua za kusajiliwa kisheria, jirani na daraja la Del Rio baada ya kuvuka Mto Rio Grande ili kuingia nchini Marekani wakitokea Ciudad Acuna, jijini Texas. **PICHA: REUTERS**

# Rusesabagina ana hatia ya ugaidi

**Kigali,** RWANDA

MWIGIZAJI maarufu katika filamu ya 'Hotel Rwanda' Paul Rusesabagina aliyejulikana kama shujaa na kuokoa maisha ya watu wengi wakati wa mauaji ya kimbari, amepatikana na hatia ya ugaidi katika mahakama.

Rusesabagina amepatikana na hatia ya kulifadhili kundi moja la waasi akiwa mafichoni ambalo liliwaua raia katika shambulio la mwaka 2018.

Familia yake imedai kwamba alichukuliwa na kurudishwa Rwanda kwa nguvu na kwamba mpendwa wao hakushtakiwa na mahakama huru. Safari ya Rusesabagina kutoka mtu aliyekuwa na sifa chungu hadi kuwa adui wa serikali, ilianza wakati alipokuwa akiikosoa sana serikali. Watoto wa Rusesabagina wanadai baba yao anaamriwa kuzungumza na alikataliwa kuwa na wanasheria huru.

Mpinzani huyo wa Rais Paul Kagame, alifahamika kwa kuokoa watu zaidi ya 1,000 wakati wa mauaji ya kimbari ya Watutsi, anashtumiwa ugaidi tangu Februari mwaka jana. Mahakama mjini Kigali jana, ilitoa hukumu hiyo dhidi ya Paul Rusesabagina, mkosoaji mkuu wa serikali ya Rwanda.

Yeye na washirika wenzake 20, walituhumiwa kwa ugaidi ambao unauhusiana na mashambulio yaliyofanywa na kundi la waasi la MRCD- FLN dhidi ya Rwanda mwaka ya 2018 na 2019.

Waendesha mashtaka waliomba hukumu ya kifungo cha maisha jela dhidi ya Rusesabagina, aliyejitoa katika kesi hiyo mara tu ilipoanza kusikilizwa kwa madai kuwa hawezi kupata haki katika mahakama za Rwanda.

Juhudi za Rusesabagina ambaye ni mwanahotelia wa zamani, zilisaidia kuwaokoa zaidi ya watu 1,200 wakati wa mauaji ya kimbari, ziliangaziwa katika filamu ya Marekani, baadaye alikuwa mkosoaji wa serikali ya Rais Kagame.

Binti yake Carine Karimba kabla ya hukumu hiyo aliiambia BBC kwamba, hawatarajii haki yoyote kutoka kwa mfumo wa haki wa Rwanda. **BBC**






MECHI KALI
HOME
NORWICH CITY
5.16 | 4.17 | 1.56
LIVERPOOL
AWAY
1 WEKA PESA.
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4 - WEKA PESA.
- FUNGUA MENYU YA HALOPESA
- CHAGUA LIPA/LIPIA BILI
- WEKA NAMBA YA KAMPUNI 150888,
KUMBUKUMBU 888.
- KISHA WEKA 500 AU ZAIDI.
SEND
2 WEKA BET.
- PIGA *150*87#
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 517,



# COMAN AGOMBEWA LIVERPOOL, CHELSEA

**LIVERPOOL,** England

MIAMBA wa Ligi Kuu England, Liverpool na Chelsea wapo kwenye rada za kumwania nyota wa Bayern Munich, Kingsley Coman, kwa mujibu wa The Mirror.

Coman ameripotiwa kutokuwa kwenye wakati mzuri kule Bayern Munich na mazungumzo kuhusu mkataba mpya yanaonekana kutokwenda vizuri.

Na sasa kwa mujibu wa ripoti hiyo, Liverpool na Chelsea zinafuatilia kwa karibu mwenendo wa kule Bavaria ili kuangalia uwezekano wa kumsajili kwa ajili ya kuimarisha vikosi vyao.

Mkataba wa sasa wa Coman na mabingwa hao wa Bundesliga unamalizika mwaka 2023 na Mfaransa huyo anaonekana kutokuwa na mpango wa kuendelea kucheza huko.

Kipindi cha dirisha la usajili la majira ya joto, nyota huyo mwenye umri wa miaka 25, alikuwa akihusishwa na Manchester United, lakini dili hili halikuweza kufanikiwa.

Lakini sasa, Liverpool na Chelsea zimeamua kuingia mazima kuhakikisha zinapata huduma ya nyota huyo.



# Messi mambo magumu PSG

**PARIS,** Ufaransa

MAURICIO Pochettino amesisitiza hakuna "kitu chochote" na Lionel Messi baada ya nyota huyo wa Paris Saint-Germain kuonyeshwa kutoridhishwa na uamuzi wa kutolewa katika mchezo wa Jumapili walioibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Lyon kwenye Ligi Kuu Ufaransa.

Messi alionyesha kushikwa na butwaa usoni mwake wakati kocha wa PSG, akimtoa nje na nafasi yake kuchukuliwa na mlinzi wa pembeni, Achraf Hakimi dakika ya 76.

Pochettino na Messi baadaye walionekana wakizungumza pamoja, ambapo alikuwa akicheza mechi yake ya kwanza nyumbani kwenye dimba la Parc des Princes baada ya kuwasili hapo akitokea Barcelona.

Messi alihusika katika mashuti sita (manne yalilenga goli, akitengeneza nafasi mbili) dhidi ya Lyon.

Mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or, Messi pia aligusa mpira mara 65 na kutengeneza pasi 48 zenye uhakika zikiwa sawa na asilimia 83.3.

Pochettino aliwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo: "Nafikiri kila mmoja anajua kwamba, tuna wachezaji wakubwa, kwenye kikosi cha watu 35.

"Tunatakiwa kufanya maamuzi, katika kila mchezo na hivyo hatuwezi kuwachezesha wote kwa wakati mmoja.

# 350,800 JACKPOT

## MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 25/09/21 | 17:00 | Leeds vs West Ham | 2.71 | 3.57 | 2.46 |
| 02. 25/09/21 | 17:00 | Watford vs Newcastle | 2.37 | 3.32 | 3.01 |
| 03. 25/09/21 | 17:00 | Blackpool vs Barnsley | 2.52 | 3.31 | 2.66 |
| 04. 25/09/21 | 17:00 | Swansea vs Huddersfield | 2.27 | 3.26 | 3.06 |
| 05. 25/09/21 | 17:00 | Nottingham vs Millwall | 2.81 | 3.05 | 2.56 |
| 06. 25/09/21 | 17:00 | Blackburn vs Cardiff | 2.34 | 3.24 | 2.95 |
| 07. 25/09/21 | 17:15 | Valencia vs Athletic Bilbao | 2.50 | 3.21 | 2.91 |
| 08. 25/09/21 | 18:00 | St Etienne vs Nice | 2.94 | 3.24 | 2.40 |
| 09. 26/09/21 | 15:00 | Mallorca vs Osasuna | 2.91 | 3.06 | 2.61 |
| 10. 26/09/21 | 16:00 | Southampton vs Wolverhampton | 2.57 | 3.22 | 2.82 |
| 11. 26/09/21 | 16:00 | Udinese vs Fiorentina | 2.66 | 3.31 | 2.66 |
| 12. 26/09/21 | 18:30 | Arsenal vs Tottenham | 2.41 | 3.17 | 3.07 |
| 13. 26/09/21 | 19:00 | Lazio vs Roma | 2.75 | 3.65 | 2.39 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMANNE - 21 - SEPTEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 4245 | Pohang Steelers vs Ulsan Hyundai | 3.05 | 3.24 | 2.18 |
| 15:00 | 1296 | ACS Somuz Falticeni vs Voluntari | 9.69 | 5.04 | 1.26 |
| 16:30 | 2279 | NK Dugopolje vs Lokomotiva Zagreb | 6.37 | 5.21 | 1.34 |
| 17:00 | 1042 | Fatih Karagumruk vs Antalyaspor | 2.07 | 3.40 | 3.35 |
| 17:00 | 2918 | Graffin Vlasim vs Sigma Olomouc | 4.25 | 3.63 | 1.71 |
| 17:00 | 4929 | Caykur Rizespor vs Altay | 2.91 | 3.30 | 2.34 |
| 18:00 | 1972 | Viktoria Plzen vs Pribram | 1.10 | 7.75 | 16.47 |
| 18:00 | 2671 | Jihlava vs Pardubice | 2.70 | 3.32 | 2.36 |
| 18:00 | 2977 | Opava vs Mlada Boleslav | 5.03 | 3.87 | 1.57 |
| 19:00 | 3499 | Alessandria vs Ascoli | 2.75 | 3.05 | 2.61 |
| 19:00 | 4339 | Benevento vs Cittadella | 2.12 | 3.06 | 3.60 |
| 19:30 | 4253 | Bologna vs Genoa | 1.99 | 3.57 | 3.67 |
| 19:45 | 5581 | Fortuna Sittard vs Ajax | 13.83 | 7.70 | 1.15 |
| 20:00 | 1453 | Besiktas vs Adana Demirspor | 1.38 | 4.84 | 6.91 |
| 20:00 | 3016 | Yeni Malatyaspor vs Sivasspor | 2.76 | 3.25 | 2.47 |
| 20:30 | 4990 | Getafe vs Atletico Madrid | 5.82 | 3.41 | 1.70 |
| 21:00 | 1750 | Dunkerque vs Toulouse | 4.93 | 3.30 | 1.76 |
| 21:00 | 1937 | Valenciennes vs Bastia | 2.81 | 3.05 | 2.56 |
| 21:00 | 2548 | AJ Auxerre vs Rodez Aveyron | 1.83 | 3.36 | 4.35 |
| 21:00 | 2615 | Amiens vs PAU FC | 2.76 | 2.91 | 2.71 |
| 21:00 | 3487 | Guingamp vs Sochaux | 2.91 | 2.86 | 2.62 |
| 21:00 | 3608 | Grenoble Foot vs Nancy | 2.00 | 3.15 | 3.89 |
| 21:00 | 5178 | AC Ajaccio vs Niort | 1.69 | 3.46 | 5.14 |
| 21:00 | 5568 | Caen vs Dijon | 2.01 | 3.21 | 3.75 |
| 21:00 | 5961 | Paris FC vs Nimes | 1.96 | 3.41 | 3.70 |
| 21:30 | 2074 | CS Mioveni vs Rapid Bucuresti | 2.95 | 3.05 | 2.34 |
| 21:30 | 2874 | Spal vs Vicenza | 1.88 | 3.26 | 4.25 |
| 21:30 | 2966 | FC Zurich vs Servette Geneva | 2.72 | 3.56 | 2.35 |
| 21:30 | 3505 | Cosenza vs Como | 2.57 | 3.16 | 2.71 |
| 21:30 | 4001 | Crotone vs Lecce | 2.39 | 3.20 | 2.91 |
| 21:30 | 4482 | Pisa vs Monza | 2.47 | 3.01 | 2.96 |
| 21:30 | 5497 | Pordenone vs Reggina | 2.71 | 3.10 | 2.61 |
| 21:45 | 1210 | Gillingham vs Charlton | 2.80 | 3.30 | 2.41 |
| 21:45 | 1619 | Norwich City vs Liverpool | 5.16 | 4.17 | 1.56 |
| 21:45 | 2143 | Burnley vs Rochdale | 1.29 | 5.31 | 9.05 |
| 21:45 | 2275 | Fiorentina vs Inter | 3.62 | 3.77 | 1.95 |
| 21:45 | 2771 | Preston vs Cheltenham | 1.52 | 4.14 | 5.72 |
| 21:45 | 2867 | Wigan vs Sunderland | 2.29 | 3.16 | 3.11 |
| 21:45 | 3202 | Atalanta vs Sassuolo | 1.55 | 4.60 | 5.20 |
| 21:45 | 3259 | Brentford vs Oldham | 1.20 | 6.31 | 11.82 |
| 21:45 | 3611 | QPR vs Everton | 4.04 | 3.70 | 1.79 |
| 21:45 | 4117 | Fulham vs Leeds | 2.65 | 3.34 | 2.51 |
| 21:45 | 4300 | Watford vs Stoke City | 1.95 | 3.30 | 3.85 |
| 21:45 | 5132 | Sheffield Utd vs Southampton | 3.54 | 3.15 | 2.11 |
| 21:45 | 5299 | Manchester City vs Wycombe | 1.06 | 9.89 | 30.43 |
| 21:45 | 5613 | Crewe vs Morecambe | 2.38 | 3.10 | 3.00 |
| 21:45 | 5853 | Portsmouth vs Plymouth | 1.81 | 3.41 | 4.35 |
| 22:00 | 2499 | Waalwick vs Willem II Tilburg | 2.56 | 3.40 | 2.56 |
| 23:00 | 2911 | Athletic Bilbao vs Rayo Vallecano | 1.98 | 3.36 | 3.97 |
| 23:00 | 5801 | Levante vs Celta Vigo | 2.46 | 3.36 | 2.86 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.



# MARTINEZ AZIKACHA ARSENAL, TOTTENHAM

**MILAN,** Italia

LAURATO Martinez amekubali kuongeza mkataba mpya na timu yake anayoitumikia kwa sasa ya Inter Milan, ambapo katika mkataba huo mpya hakuna kipengele cha kuruhusiwa kuondoka.

Martinez ambaye alikuwa anafuatiliwa na klabu za Arsenal na Tottenham katika dirisha la majira ya kiangazi, sasa atabaki hapo Milan, kwa mujibu wa ripoti za nchini Italia.

Kwa sasa usajili wa Martinez utakuwa mgumu kutokana na kukubali kuongeza mkataba mwingine, ambao utamuweka na kufungumana na klabu kwa muda mrefu kukiwa hakuna kipengele kitakacho muwezesha kuondoka.

Martinez mwenye umri wa miaka 24, alikuwa ana thamani ya pauni milioni 55, wakati akiwa amebakisha miaka miwili katika mkataba wake kwenye dirisha la usajili lililopita.

Na kwa , kwa sasa thamani yake itapanda zaidi kulingana na mkataba, ambao atakwenda kutia kusaini, ingawa bado haijawekwa wazi ni lini, lakini imesemwa ni siku chache zijazo.



# Countinho sasa tumaini jipya Barca

**BARCELONA,** Hispania

PHILIPE Countinho sasa yupo katika nafasi ya kupata wakati mwingi zaidi wa kucheza na kurejesha umuhimu wake msimu huu, kwa mujibu wa Marca.

Nyota huyu wa Brazil amekuwa na kipindi kigumu tangu alipowasili klabuni hapo, kwa uhamisho wa fedha nyingi hapo Camp Nou mwaka 2018, akitokea Liverpool.

Alitumia mwaka mmoja kwa mkopo kule Bayern Munich, akifanikiwa kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, na kujikuta kwenye mkwamo wa majeraha na hakuwa kwenye kiwango kizuri.

Countinho sasa amerejea akiwa fiti na tayari ameshaanza kucheza mechi na kikosi chake cha Barcelona akitokea benchi kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, ambayo walipoteza, dhidi ya Bayern kwa mabao 3-0.

Kwa mujibu wa chapisho la Marca, Countinho sasa anatarajiwa kucheza mechi nyingi zaidi chini ya kocha Ronald Koeman, kikosi ambacho kwa siku za hivi karibuni kimeonekana kupungua ubora.

Countinho anamaliza mkataba wake wa sasa na Barcelona mwaka 2023, na msimu ujao utakuwa muhimu zaidi katika maisha yake ya soka, ili kujua kesho yake.

**HABARI MICHEZO**

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SOLSKJAER AKUNWA UBORA WA DE GEA MAN UNITED

**●●● Ninaimani na David na nimemwona yeye akiokoa penalti mara nyingi, aliokoa dhidi...**

**LONDON,** England

OLE Gunnar Solskjaer amemsifia David de Gea baada ya kuokoa penalti dakika ya mwisho wakati Manchester United ikiibuka na ushindi dhidi ya West Ham, huku akikataa kuzungumzia matumaini ya ubingwa wa Ligi Kuu England.

**Golikipa huyo wa United, De Gea aliokoa penalti hiyo kuwasaidia 'Mashetani Wekundu' kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya West Ham, Jumapili kwenye Uwanja wa London.**

Jesse Lingard alifunga bao la pili la ushindi dakika ya 89 baada ya mchezaji mwenzake, Cristiano Ronaldo kufunga mapema bao la kusawazisha wakati Man United ikiwa nyuma kwa bao 1-0 lililofungwa na Said Benrahma.

De Gea aliokoa penalti hiyo iliyopigwa na Mark Noble katika muda wa nyongeza dakika ya 95 - na raia huyo wa Hispania alimaliza ukame wa kutookoa penalti tangu Aprili 2016.

De Gea sasa ameokoa penalti tatu na kufungwa 28 kwenye Ligi Kuu; akishindwa kuokoa 21 mfululizo kwenye mashindano hayo kabla ya kukataa hiyo ya Noble.

De Gea kwa muda majaliwa yake ndani ya Old Trafford yalikuwa shakani, ambapo ujio wa Dean Henderson msimu uliopita ulizidisha uvumi wa yeye kuondoka, lakini Solskjaer alimsifia kipa huyo mwenye umri wa miaka 30.

"Nina imani na David na nimemuona yeye akiokoa penalti mara nyingi," alisema Solskjaer akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Aliokoa dhidi ya Crystal Palace msimu uliopita, na sasa aliibuka tena shujaa kwenye mchezo huu.

"Nimemuona Mark Noble akifunga penalti nyingi, hivyo nilihisi kuwa hata ile asingekosa, lakini bahati nzuri ni kwamba David aliendeleza kiwango chake bora."

## ZISIKUPITE

### BARCELONA YATAKA NYOTA

BARCELONA wanajiandaa kuwasilisha ofa za kuwanunua mshambuliaji wa Borussia Dortmund na Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 21, nyota wa Ufaransa na Manchester United, Paul Pogba, 28, na mchezaji wa Hispania, Dani Olmo, 23. ***(Mundo Deportivo)***

### POGBA MSHAHARA JUU

HUKU mkataba wa Paul Pogba na Manchester United ukikamilika majira yajayo ya joto, klabu hiyo imejiandaa kutoa ofa ya mshahara wa pauni 400,000 kwa wiki kumfanya kuwa mchezaji anayelipwa mshahara wa juu zaidi katika Ligi Kuu England wakati wote. ***(Express)***

### LINGARD KUUZWA JANUARI

KIUNGO Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 28 na beki Eric Bailly, 27, ni miongoni mwa wachezaji saba ambao wanaweza kuuzwa na Manchester United Januari. ***(Sun)***

### TCHOUAMENI ATAKIWA CHELSEA

CHELSEA itakabiliana ana kwa ana na Juventus katika mbio za kusaka saini ya kiungo wa chini ya umri wa miaka 21 wa Ufaransa na Monaco, Aurelien Tchouameni, 21, Januari. ***(Tuttomercatoweb)***

### COMAN AGEUKA LULU

LIVERPOOL, Tottenham na Juventus wamepania kumpigania winga wa Bayern Munich na Ufaransa, Kingsley Coman mwenye umri wa miaka 25. ***(Fichajes)***

### KANE NA UHAMISHO SPURS

MSHAMBULIAJI wa Tottenham, Harry Kane, 28, anaweza kuwa bado anahisi athari za uhamisho wake ulioshindwa kufanyika Manchester City msimu huu wa majira ya joto. ***(TalkSport)***

### JUVE NA DONNARUMMA

JUVENTUS walikuwa wamepanga kumsajili Gianluigi Donnarumma, 22 kwa uhamisho huru kutoka AC Milan msimu huu wa majira ya joto, lakini walilazimika kujiondoa kwa sababu za kifedha, na kuiruhusu Paris St-Germain kumchukua. ***(Goal)***

### LEONARDO NA DAU LA MESSI

MKURUGENZI wa michezo wa PSG, Leonardo amepuuza maoni kwamba nyota wa Argentina, Lionel Messi,34, atapata zaidi ya pauni milioni 30 kwa msimu wakati wa mkataba wake wa miaka mitatu. ***(Mail)***

### KOEMAN HAJUI HATIMA

BOSI wa Barcelona, Ronald Koeman hajui hatima yake iko vipi wakati kukiwa na ripoti kwamba Rais Joan Laporta anaunda orodha ya watu watakaochukua usukani wa klabu hiyo. ***(Express)***

### WAJITOSA KWA COMAN

CHELSEA pia inavutiwa na Kingsley Coman baada ya mkurugenzi wa zamani wa michezo wa Bayern Munich kumtaka aondoke klabuni hapo. ***(Mirror)***

## KMKM na sababu kutupwa nje CAF

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BAADA ya kufurushwa nje kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha Mkuu wa KMKM, Ame Msimu, amesema kutolewa kwao hakutokani na uwezo mkubwa wa wapinzani wao, bali ni makosa madogo madogo, ambayo waliyafanya hivyo kuadhibiwa.

KMKM imetolewa katika michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), baada ya kupoteza michezo yote miwili kwa kufungwa jumla ya mabao 4-0, dhidi ya Al-Ittihad ya Libya.

Katika mchezo wa marudiano uliopigwa juzi, Jumapili nchini Tunisia kutokana na hali ya usalama Libya kutokuwa shwari, KMKM ilikubali kichapo cha mabao 2-0 sawa na ilichokipata kwenye mechi ya awali ikiwa nyumbani Uwanja wa Amaan wiki moja iliyopita.

"Wachezaji walicheza vizuri na walijituma, lakini kama ilivyo mchezo wa soka, kosa dogo unalolifanya basi linampa faida mpinzani wako, ndivyo ilivyotokea," alisema.

## Tamasha la Wachina kufanyika mtandaoni

**Na Faustine Feliciane**

TAMASHA la kuadhimisha mwaka wa Wachina 'China Mid-Autumn Festival 2021', ambalo hufanyika kila mwaka mwishoni mwa Septemba au mwanzoni mwa Oktoba, linafanyika leo kupitia njia ya mtandao.

Tamasha hilo linalohusisha Mambo mbalimbali ya kitamaduni ya Wachina kwa mwaka huu linafanyika tofauti kutokana na janga la mlipuko wa virusi vya corona.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi wa Kituo cha Utamaduni cha China nchini, Wang Siping, alisema tamasha la mwaka huu wanaliadhimisha kwa kutoa misaada kwa watu mbalimbali wenye mahitaji.

"Mwaka huu tamasha hili linafanyika tofauti kidogo, hatutakutana kama ilivyokuwa miaka ya nyuma kutokana na mlipuko wa corona, tutaadhimisha kwa njia ya mtandao, ambapo watu mbalimbali Wachina watajirekodi na kutuma video zao kwenye mtandao wetu," alisema Siping.

Alisema tamasha hilo litaadhimishwa kwa siku tatu, ambapo mambo mbalimbali yatafanyika kuonyesha utamaduni wa Wachina ikiwamo mapishi ya vyakula vya Kichina, kucheza Ngoma za Kichina na mengineyo.

# OKWI SASA AITAKA SIMBA

**Na Shufaa Lyimo**

MSHAMBULIAJI wa zamani wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Emmanuel Okwi, ambaye kwa sasa ni mchezaji huru kutokana na kumaliza mkataba wake na Al Ittihad Alexandria Club ya Misri, amesema atafurahi endapo atapata nafasi ya kusajiliwa kwa mara nyingine na Wekundu wa Msimbazi hao.

Okwi juzi alihudhuria Tamasha la Simba Day lililofanyika Uwanja wa Benjamin Mkapa na kuibua shangwe kwa mashabiki wa timu hiyo wakati akizunguka uwanjani kuwasalimia.

Akizungumza na Nipashe uwanjani hapo, Okwi alisema amelazimika kuhudhuria Tamasha la Simba Day kutokana na mapenzi makubwa aliyo nayo kwa timu hiyo.

> **"Nitafurahi kama nitapata tena nafasi ya kusajiliwa katika kikosi cha Simba kwenye usajili wa dirisha dogo, kwa sababu kwa sasa sina timu yoyote, mkataba na timu yangu niliyokuwa ninaichezea umeisha na sijatia saini tena," alisema Okwi.**

Akitoa tathimini yake kuhusu kikosi cha Simba, alisema kwa sasa imebadilika kwa kiasi kikubwa tofauti na ilivyokuwa kipindi anaichezea kutokana na kuwa na wachezaji wenye viwango vya hali ya juu.

Aidha, alisema pamoja na ubora ilioku wa nao msimu ulioisha, amefurahishwa na usajili uliofanywa msimu huu kwa kusajili wachezaji wengi chipukizi, ambao wanaonekana kuwa na kasi kubwa uwanjani, jambo ambalo litazidi kuongeza ushindani wa namba kwa kila mchezaji.

Alisema soka la Afrika Mashariki limepanda kwa kiasi kikubwa kitu, ambacho kimesaidia kupatikana kwa wadhamini mbalimbali.

"Nimefurahishwa pia na mapokezi makubwa waliyonionyesha mashabiki wangu katika Simba Day, binafsi nimefurahishwa na kitendo hicho, sijategemea kama ningefanyiwa hivyo,"alisema.



Mnadhimu Mkuu wa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ), Luteni Jenerali Mathew Edwardo Mkingule, akimkabidhi kikombe na zawadi mshindi wa jumla wa mashindano ya Kombe la Mkuu wa Majeshi 2021, Victor Joseph, yaliyofanyika viwanja vya TPDF Golf Lugalo na kudhaminiwa na Benki ya NMB. Kushoto ni Afisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa NMB (Chief of Retail Banking), Filbert Mponzi na Kulia ni Afisa Mkuu wa Biashara na Serikali (Chief Wholesale Banking), Alfred Shayo na wapili kutoka kulia ni Mwenyekiti wa Gofu Lugalo, Brigedia Jenerali Mstaafu Michael Luongo. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *NMB yakabidhi zawadi mshindi wa CDF Trophy*

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imelipongeza Jeshi la Wananchi la Tanzania (JWTZ), kwa namna linavyozidi kuutangaza mchezo wa gofu nchini.

Pongezi hizo zilitolewa juzi usiku na Afisa Mkuu wa Wateja Wakubwa na Serikali wa Benki ya NMB, Alfred Shayo, wakati wa tafrija ya utoaji zawadi kwa washindi wa mashindano ya NMB CDF Trophy, yaliyofanyika viwanja vya gofu vya Lugalo.

Shayo alisema mashindano ya Kombe ya Mkuu wa Majeshi ni moja kati ya michuano mikubwa ya gofu nchini, yamevutia watu wengi wakiwamo wanajeshi na raia na kufanya wachezaji kuongezeka.

"Michezo sasa ni ajira yenye kulipa sana duniani, hivyo kwa kuzalisha wacheza gofu wengi zaidi, tunasaidia kuzalisha ajira kwa Watanzania wenzetu.

"Kwa miaka sita sasa, tumekuwa pamoja na niwahakikishieni tu, Benki ya NMB bado ipo pamoja nanyi katika mashindano haya na tutazidi kuboresha udhamini wetu kwa kadri mahitaji yatakavyoongezeka," alisema Shayo

Akizungumzia udhamini wa benki hiyo, alisema imegharamia vifaa na fedha taslimu, kwa ajili ya kununua zawadi zenye thamani ya shilingi milioni 60.

Aidha, Shayo alisema Benki ya NMB imekuwa mdau wa michezo ya aina mbalimbali nchini, "kwa mchezo wa gofu tumekuwa washirika wa muda mrefu wa Klabu ya Gofu ya Lugalo na wadau wakubwa wa mashindano haya ya mkuu wa majeshi".

Katika mashindano hayo yaliyoshirikisha wachezaji zaidi ya 150 kutoka klabu zote nchini, nahodha wa timu ya Taifa ya Tanzania, Victor Joseph, aliibuka mshindi baada ya kupata grosi 141 akifuatiwa na Aldo Gandye, aliyepata grosi 154.

Kwa upande wa upigaji wa mipira ya neti, Amri Kangajaka aliibuka mshindi wa jumla, baada ya kupiga mikwaju ya neti 141 akifuatiwa na Elisha Fadhili, aliyepata neti 143.

Upande wa Divison A, Petar Fiwa, alishinda baada ya kupiga mikwaju ya neti 150 akifuatiwa na Damasi Gaitana aliyepata neti 152, huku kwa Division B, Lunacho Lugome akiibuka mshindi baada ya kupiga mikwaju ya neti 145, akifuatiwa na Hussein Dewji aliyepata neti 145.

Dision C, Vitalis Magere alishinda kwa kupiga mikwaju ya neti 149 akifuatiwa na Dotto Bahenge aliyepata neti 152 huku kwa upande wa wanawake nafasi hiyo ikichukuliwa Zuhura Shemdolwa aliyepata neti 143.

Kwa upande wa wachezaji wa kulipwa nafasi ya kwanza ilichuliwa na Frank Mwinuka aliyepata grosi 140, huku Abdalah Yusuph akiwa wa pili baada ya kupata grosi 150.

# Michezo

Jumanne Septemba 21, 2021

Nipashe




Solskjaer akunwa ubora wa De Gea UKURASA 22

MAESTRO...



Kiungo wa Simba, Rally Bwalya, akimiliki mpira dhidi ya wachezaji wa TP Mazembe kwenye mechi ya kirafiki ya Simba Day, iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi na miamba hiyo DR Congo kuibuka na ushindi wa bao 1-0. **NA MPIGAPICHA WETU**

# NABI AMTAJA MAYELE, DJUMA SIMBA, YANGA

## ●●● Asema maingizo mapya muhimu Jumamosi, atoa pia sababu tatu kipigo cha Nigeria...

**Na Adam Fungamwango**

HUKU akitaja sababu zilizochangia kikosi chake kutupwa nje kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya awali, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema mchezo wa Ngao ya Jamii dhidi ya Simba Jumamosi, hautakuwa rahisi, lakini ana matumaini ya kufanya vizuri kwa kuwa atakuwa na maingizo mapya kikosini.

**Yanga juzi ikiwa ugenini nchini Nigeria, ilikubali tena kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Rivers United kama ilivyokuwa wiki moja iliyopita katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, hivyo kutolewa kwenye michuano hiyo ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa jumla ya mabao 2-0.**

Hivyo, kwa sasa Yanga ambayo imerejea nchini jana ikitokea Nigeria, inajiandaa na mechi ya Ngao ya Jamii dhidi ya Simba, mchezo ambao utapigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumamosi ukiwa ni maalum kwa ajili ya kufungua msimu mpya wa Ligi Kuu Bara 2021/22.

Akizungumza na mwandishi wetu baada ya kufurushwa nje ya michuano hiyo ya CAF, Nabi alisema mchezo huo umepita na sasa anaumulika ulio mbele yao dhidi ya Simba Jumamosi ambao anaamini utakuwa mgumu.

"Kuhusu mechi ya Jumamosi, itakuwa tofauti kwa kuwa nitakuwa na maingizo mengine kama Djuma [Shabani], Mayele [Fiston], ambao wanaruhusiwa kucheza mechi hiyo, hivyo wataongeza nguvu katika kikosi," alisema.

Kwa upande wa sababu ya kutolewa mapema katika michuano hiyo ya CAF, Nabi alisema kubwa ni kutokuwa na maandalizi mazuri ya mwanzo wa msimu 'pre season', lakini wakikabiliwa na matatizo mengi ya baadhi ya wachezaji kukosa vibali, pamoja na kuathiriwa kisaikolojia na wapinzani wao kuwasingizia baadhi ya wachezaji wao kuwa wana maambukizi wa ugonjwa wa COVID-19.

Nabi alisema sababu kubwa ya kwanza ni kikosi kutokuwa na maandalizi mazuri ya msimu ambayo yamesababisha kutokuwa na stamina na pumzi, hasa kipindi cha pili.

"Kipindi cha kwanza tulicheza vizuri sana, tatizo pekee lilikuwa ni kufunga magoli. Kipindi cha pili nguvu ilipungua, hatukuwa na pumzi na stamina ilikuwa ndogo na haya yamesababishwa na kutopata maandalizi ya kutosha ya msimu.

"Pili ni kwamba wapinzani wetu walitutoa kwenye mchezo, baada ya kutuambia kuwa kuna baadhi ya wachezaji wana maambukizo ya corona, hii ilitufanya kutuondoa kwenye mchezo, kwani hata walivyokubali, lakini tayari kisaikolojia walikuwa wametuathiri," alisema kocha Nabi.

Kocha huyo pia ameeleza pia sababu nyingine ni kukosekana kwa baadhi ya wachezaji wake tegemeo ambao alitarajia wangekuwa sehemu ya kikosi kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, lakini hawakuwapo kutokana na kukosa Hati za Uhamisho wa Kimataifa (ITC). Wachezaji hao ni Mayele, Djuma na Khalid Aucho.

"Kwa hiyo hapo utaona kuwa timu ilikuwa ina bahati mbaya, ilikuwa inakabiliwa na matatizo mengi, lakini kwa sasa naangalia mechi inayofuata ya Ngao ya Jamii dhidi ya Simba na wachezaji hao watakuwapo," alisema.

## Gomes: Sikutaka matokeo kwa TP Mazembe

**Na Saada Akida**

BAADA ya kukubali kipigo cha bao 1-0 dhidi ya TP Mazembe ya DR Congo kwenye mechi ya kirafiki iliyopigwa katika Tamasha la Simba Day, Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi, Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, amesema kuna kitu alichokuwa akihitaji kukiangalia zaidi kikosini kuliko matokeo ya ushindi.

Akizungumza na Nipashe baada ya mchezo huo, Gomes alisema kwa kiasi kikubwa wachezaji wake walifanya kile ambacho amewaelekeza, isipokuwa kuna kasoro chache ambazo sasa anakwenda kuzifanyia kazi kabla ya kukutana na Yanga Jumamosi wiki hii kwenye mchezo wa Ngao ya Jamii maalum kwa ajili ya ufunguzi wa msimu mpya wa Ligi Kuu Bara 2021/22.

"Ulikuwa mchezo mzuri sana kwetu, binafsi sikuwa natafuta zaidi matokeo na badala yake nilichokuwa nakiangalia ni namna wachezaji wanavyoweza kutekeleza kile nilichowafundisha na kwa kiasi kikubwa nimeona juhudi zao.

"Kama uliangalia vizuri ule mchezo tulipoteza nafasi kadhaa nzuri ambazo endapo tungezitumia vizuri, tungeweza kupata ushindi, hivyo tunakwenda kurekebisha haya mapungufu, ili kufanya vizuri zaidi michezo yetu inayokuja," alisema.

"TP Mazembe walikuwa na kiwango bora kuliko sisi, tukumbuke tuliwahi kucheza nao katika mchezo wa ushindani, safari hii wamerudia tena wakiwa bora zaidi yetu, nadhani hii itatusaidia sana," alisema Gomes.

Gomes alisema mchezo huo utakuwa umewapa somo kubwa wachezaji wake kuelekea mechi dhidi ya Yanga Jumamosi wiki hii huku akidai kuwa, ana imani kubwa na kikosi chake.

Wakati Gomes akisema hayo, Kocha Mkuu wa TP Mazembe, Franck Dumas, alisema: "Tumewafunga lakini haikuwa kazi nyepesi, hawa jamaa ni wapambanaji sana, ndiyo maana katika misimu hii ya hivi karibuni wamekuwa wakipata matokeo mazuri michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika."

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >